**MADALALI** wamkaba mwandishi kwenye bomoabomoa Dar

UKURASA 3

**NECTA** yafafanua kilichobadilika kwenye Mtihani wa Darasa la VII

UKURASA 4



**KAMALA**, Trump warushiana vijembe, hali ya hewa yachafuka

UKURASA 19


ama

ALHAMISI SEPTEMBA 12, 2024

AFYA NA MAZINGIRA

Bingwa afya akili, awaonyesha vijana njia sahihi kukwepa madhara ngono

JANABI, TIBA PUTO NA MAMBO YAKE

Vicent alivyotimiza lengo kutoka kilo 150 hadi 90; kiuno chake inchi 50 hadi 36

VIFO UZAZI VYAPUNGUA 80%

Samia akiinakishi afya kupitia MMAM ya JK; Mama & Mtoto, Afya ya Msingi

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Septemba 12, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581797

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Ahadi tano za Samia kwa wahitimu la VII

UKURASA 2

## MAAJABU YA PUTO

### Kutoka kibonge kilo 150 hadi 99, robo ya kiuno yaondoka

UKURASA 12 & 13



ZAMANI



SASA



Mabaunsa wa Kampuni ya Bilo Star Debt Collection Co. Ltd, wakiwatoa nje wapangaji waliokuwa wakiishi katika nyumba kitalu namba 266, Barabara ya Ally Khan, eneo la Upanga Magharibi, jijini Dar es Salaam jana inayosemekana kuwa na mgogoro. **Habari Uk. 3. PICHA: IMANI NATHANIEL**

KIFO CHA KIBAO

## Lissu: Vyombo vya dola vichunguzwe kimataifa

**TLS**, wadau waibuka na hoja sita...Endelea Uk. 3



Mwabukusi

Lissu

**MICHEZO** **MOROCCO ATOA SIRI USHINDI WA STARS** UK 24

**MAONI, KATUNI UK.6**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Mratibu wa FISH4ACP, Hashim Muumini, kuhusu teknolojia ya ukaushaji wa dagaa. Pembeni ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ahadi tano za Samia kwa wahitimu la VII

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametoa ahadi tano kwa wanafunzi 1,230,780 wanaofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi unaomalizika leo nchini, huku akisema ni zawadi kwao ambayo serikali inahakikisha inatimia.

Katika taarifa aliyoiandika kwenye WhatsApp Channel, Rais Samia alisema anawatakia kila la heri wanafunzi wa darasa la saba watakaomaliza elimu ya msingi leo.

"Mnatoka katika hatua moja ya elimu na malezi kwenda nyingine katika safari yenu ya kujiandaa kutoa mchango wenu wa maendeleo kwa taifa letu. Serikali imeandaa mazingira sahihi ili kufikia lengo,"alisema.

Alisema ahadi yake kwa wanafunzi hao katika safari ya elimu na maisha ambayo tayari inatekelezwa uhakika wa kupata nafasi ya kujiunga kidato cha kwanza 2025 kwa kila atakayefaulu.

Nyingine ni miaka minne ya sekondari ya awali bila ada; miaka miwili ya kidato cha tano na sita bila ada; chuo cha ufundi katika kila wilaya kwa watakaochagua njia hiyo; na mikopo ya elimu ya juu kwa watakaofaulu kwenda vyuo vikuu.

Alisema ahadi hiyo inakwenda sambamba na kuendelea kuboresha sera za uchumi, ili kuzalisha fursa zaidi kwa kila mmoja kadiri wanavyoendelea kukua na kuingia katika nguvu kazi.

Kupitia Waraka wa Elimu Namba Tatu wa mwaka 2016, serikali ilitoa elimu ya awali hadi kidato cha nne bila malipo huku kupitia Waraka wa Elimu Namba Tano wa mwaka 2022, iliondoa ada kwa kidato cha tano na sita katika mfumo wa umma.

Kuondolewa kwa malipo hayo na kutolewa mikopo ya elimu ya juu ni utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mfunzo ya mwaka 2014 yenye lengo la kuhakikisha kuwa watoto wote wenye rika lengwa wanapata elimu bila kikwazo.

Aidha, ujenzi wa vyuo vya ufundi ni utekelezaji wa sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 ya kuwapatia vijana elimu bora na ujuzi stahiki, ili kuinua kiwango cha ujuzi wa nguvu kazi na kukidhi mahitaji ya soko.

Akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2023/24, Waziri Prof. Adolf Mkenda alisema serikali itaongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu 223,201 hadi 252,245.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Dk. Said Ally Mohamed, kati ya watahiniwa waliosajiliwa wavulana ni 564,176 sawa na asilimia 45.84 na wasichana ni 666.604 sawa na asilimia 54.16.

Alisema watahiniwa 1,158,862 sawa na asilimia 94.16 watafanya mtihani kwa Lugha ya Kiswahili na 71,918 sawa na asilimia 5.84 watafanya kwa lugha ya Kiingereza, lugha walioitumia wakati wa kujifunza.

Alisema watahiniwa wenye mahitaji maalumu waliosajiliwa ni 4,583, kati yao 98 ni wasioona, 1,402 wenye uoni hafifu,

1,067 wenye uziwi, 486 ni wenye ulemavu wa akili na 1,530 ni wenye ulemavu wa viungo.

Pia alisema mitihani hiyo itajumuisha masomo sita ambayo ni Kiswahili, English Language, Sayansi na Teknolojia, Hisabati, Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi na Uraia na Maarifa.


**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI YA SIKU 14/MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **NCBA Bank Tanzania Limited** tunatoa Notisi ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa mdaiwa tajwa hapo chini kwenye jedwalii alipe deni analodaiwa na benki Pamoja na riba. Kushindwa kufanya hivyo mali iliyowekwa kama dhamana itauzwa kwa njia ya mnada wa Hadhara kufidia deni hilo.Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo tarehe na muda kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|
| 1. | SETH FUEL (T) LTD / CHRISTINA NTUMIGWA MWAKIFULEFULE | NYUMBA YA MAKAZI YENYE HATI NA. 185383 KIWANJA NA. 661 KITALU 'C' ENEO LA KISUKULU MANISPAA YA ILALA YENYE JINA LA CHRISTINA NTUMIGWA MWAKIFULEFULE ILIYODHAMINI MKOPO WA SETH FUEL (T) LTD | 28-9 -2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | LUSEKELO JOSEPH KASSANGA | NYUMBA YA MAKAZI YENYE HATI NA. 125899 KIWANJA NA. 1 KITALU 'F' ENEO LA MALAMBA MAWILI MANISPAA YA UBUNGO YENYE JINA LA LUSEKELO JOSEPH KASSANGA | 05-10-2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ 765 363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**NCBA Bank Tanzania Limited**
**P. O. BOX 20268, DAR ES SALAAM**
**Tel: +255 22 2130113 / 255 22 2125710**


# PM: Uvuvi waingiza mapato trilioni 2.9/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema sekta ya uvuvi inaingiza mapato ya Sh. trilioni 2.94 kwa mwaka na imekuwa ikikua kwa wastani wa asilimia 1.9.

"Wastani wa uzalishaji wa samaki kwa mwaka hapa nchini unafikia tani 472,579, huku 429,168 sawa na asilimia 91 zikitokana na uvuvi wa kawaida wa kutumia vyanzo vya asili ndani ya bahari, mito na maziwa na tani 43,411 sawa na asilimia tisa zikitokana na ufugaji wa samaki."

Alisema hayo wakati akifungua Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pasifiki (OACPS), wanaohusika na masuala ya uvuvi, bahari, maziwa na mito ulioanza jana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza kwa niaba ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu alisema kila siku watu 230,000 wanajishughulisha na uvuvi mdogo na Watanzania milioni sita wamepata ajira zisizo za moja kwa moja kwenye sekta hiyo. "Uvuvi mdogo mdogo unachangia zaidi ya asilimia 95 ya mavuno yote ya samaki nchini," amesema.

Akielezea fursa za uwekezaji kwenye ufugaji wa samaki, alisema Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuendeleza sekta hiyo kutokana na rasilimali kubwa za maji ilizonazo ikiwa ni pamoja na Bahari ya Hindi, maziwa, mito, mabwawa mengi ya asili na yaliyojengwa na binadamu.

"Eneo Maalum la Kiuchumi la Tanzania ni fursa kubwa ya uwekezaji kupitia ununuzi wa meli za uvuvi, uwekezaji wa huduma za meli, usambazaji wa vifaa vya uvuvi, usambazaji wa chakula (maji, chakula na matunda), kuongeza thamani na usindikaji, utafiti na ulinzi wa baharini na angani."

Alizitaja fursa nyingine za uwekezaji kuwa ni pamoja na uvuvi wa kina kirefu kwa ajili ya samaki aina ya tuna; kilimo cha mwani; uzalishaji wa vifaranga na chakula cha samaki.

Akielezea matarajio ya mkutano huo, Waziri Mkuu amesema mkutano huo utatoa mwongozo wa kimkakati kwenye vikao vya juu vya maamuzi vya Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pasifiki ili kuboresha usimamizi wa bahari, uvuvi na ufugaji endelevu wa samaki.

Amesema Tanzania itaendelea kuunga mkono malengo ya umoja huo hasa katika kukuza uchumi wa bluu na maendeleo endelevu. "Uamuzi huu utasaidia kuimarisha malengo ya umoja wetu na kuboresha ustawi wa nchi wanachama pamoja na wananchi wake. Umoja huu ni miongoni mwa majukwaa ya msingi sana yanayoweza kuchangia mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu ya Tanzania."

Umoja wa Nchi za Afrika, Karibian na Pasifiki (OACPS) unajumuisha nchi wanachama 79 ambapo 48 kati ya hizo zinatoka Bara la Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, nchi 16 zinatoka Caribbean na nchi 15 zinatoka Pasifiki. Umoja huu ambao unalenga kuchochea maendeleo endelevu, kuondoa umaskini na kukuza fursa za kibiashara miongoni mwa wanachama wake umetokana na kundi la nchi za Afrika, Caribbean na Pasifiki (ACP) ambalo lilianzishwa kwa makubaliano ya Georgetown ya mwaka 1975.

Mapema, akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na washiriki wa mkutano huo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema umoja huo ni kiungo muhimu cha OACPS katika kukuza ushirikiano kati ya nchi wanachama na usimamizi wa rasilimali za bahari.



Magari yakipita kwa shida kwenye shimo lililoko katika kona ya makutano ya Barabara za Bagamoyo na Motisun, eneo maarufu la Mwenge ITV, Dar es Salaam jana. Shimo hilo, lipo kwa muda mrefu sasa na kusababisha usumbufu mkubwa kwa vyombo vya moto. **PICHA: JOHN BADI**

## KIFO CHA KIBAO

# Lissu: Vyombo vya dola vichunguzwe kimataifa

**Na Jenifer Gilla**

TAASISI mbalimbali zimeendelea kutoa matamko kulaani kuuawa kwa Mjumbe wa Sekretarieti ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ally Kibao, huku Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, akisema vyombo vya usalama havipaswi kuchunguza matukio ya utekaji, utesaji na mauaji.

Pia amesema vyombo hivyo vya usalama havitakiwi kuchunguza kwa kuwa vinashutumiwa jambo ambalo halitaweka imani kwa wananchi.

Lissu alishauri kuundwa timu ya wataalamu wa kimataifa ambao hawajaegemea upande wowote kufanya uchunguzi huo.

Akizungumza na Jambo TV katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (JNIA), baada ya kuwasili kutoka Ubelgiji, Lissu alisema utaratibu unaofaa katika uchunguzi huo ni kuleta timu za kimataifa na si polisi kujichunguza.

Kauli ya Lissu imekuja zikiwa ni siku nne tangu Rais Samia Suluhu Hassan kuliagiza Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi juu ya kifo cha Kibao na kupewa taarifa za kina juu ya tukio hilo.

Rais alisema Tanzania inaongozwa na misingi ya kidemokrasia, hivyo kila raia ana haki ya kuishi na serikali haitavumilia vitendo vya kikatili vya namna hiyo.

Lissu alisema vyombo vya usalama vinahitaji kuchunguzwa na kusafishwa ili vitekeleze majukumu ya kuimarisha ulinzi na usalama inavyostahili na si kujichunguza.

Alisema njia pekee inayofaa kutumika ni kuleta timu ya kimataifa kuchunguza matukio hayo kwa kuwa hao ni watu wanaoaminika kuitenda kazi hiyo vizuri bila kuegemea upande wowote.

"Idara ya Usalama wa Taifa anayoiongoza mwenyewe (Rais Samia), Jeshi la Polisi ndio watuhumiwa wa kwanza. Watajichunguzaje? Lini Jeshi la Polisi limeshawahi kuchunguza chochote cha mambo haya?" alihoji.

Alisema utaratibu wa kuundwa kwa Tume ya Kijaji ya Uchunguzi ni mzuri ingawa changamoto yake ni kuwa tume hiyo inaripoti kwa rais na matokeo yanakuwa siri hivyo njia hiyo haifai kutumika.

**JAJI AUNGA MKONO**

Akizungumza katika mkutano wa wadau wa haki za binadamu, Jaji (mstaafu) Thomas Mihayo, alishauri kuanzishwa kwa Mahakama Maalumu ya Uchunguzi itakayokuwa na mamlaka kamili ya kuchunguza matukio hayo kwa kina badala ya tume ya uchunguzi.

Alisema chombo hicho kitakuwa na nguvu zaidi kuliko tume ya uchunguzi kwani itaweza kukusanya na kuhoji mashahidi, na kutoa maamuzi yenye msingi wa kisheria.

Jaji Mohayo alisema tume za uchunguzi mara nyingi hazina mamlaka kamili na zinategemea ripoti zao kuwasilishwa kwa vyombo vingine vya dola, hali inayoweza kuchelewesha haki na kusababisha matokeo yasiyofaa.

**KAULI YA MISA- TAN**

Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika tawi la Tanzania (MISA-TAN), ililaani vikali wimbi linaloendelea la utekaji wa mauaji ya wananchi wasiokuwa na hatia nchini hasa tukio la utekwaji na mauaji ya kada huyo wa CHADEMA.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Bodi ya Uongozi wa Taasisi hiyo, matendo hayo ni kielelezo tosha cha uvunjwaji mkubwa wa sheria na ukiukwaji wa haki za binadamu na hasa haki ya msingi ya kuishi.

Aidha, waliiomba serikali kuchukulia kwa uzito wimbi hili na kutengeneza mikakati mahsusi ya kiuchunguzi, ikiwamo kuunda tume huru ya kijaji ili kufuatilia mwenendo huu haramu katika nchi hiyo.

"Jambo hili la utekaji na mauaji ambao yanafanywa kwa wanasiasa, wafanyabishara na raia wengine yanatengeneza chuki miongoni mwa wananchi na kunyooshewa vidole vyombo vya dola kama Jeshi la Polisi kuhusika na hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya matukio yamehusisha taasisi hiyo ya ulinzi hapa nchini," ilisema taarifa hiyo.

Pia iliisihi serikali kuchukua hatua hizo kwa haraka iwezekanavyo ili kutoruhusu uharibifu mkubwa kuendelea kwenye jamii hasa nchi inapoelekea kwenye matukio makubwa ya kidemokrasia ya uchaguzi wa serikali za mtaa Novemba, mwaka huu na uchaguzi mkuu 2025.

Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kimeunga mkono hoja ya kuundwa kwa tume huru ya kuchunguza matukio hayo ili kupata suluhu ya kudumu kwa lengo la kurejesha imani ya wananchi juu ya uhuru wao na haki za msingi za kikatiba ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi ambayo sasa iko mashakani.

Rais wa TLS, Boniface Mwabukusi, alisema chama hicho kinatoa wito Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camilus Wambura na Mkuu wa Mafunzo wa Jeshi la Polisi wawajibike.

Aidha, alilitaka Jeshi la Polisi lihakikishe kamba linatoa taarifa sahihi kwa umma dhidi ya watu wote waliochukuliwa na kutekwa kinyume na sheria kwa kueleza taratibu walizochukua mpaka kuhakikisha watu hao wanapatikana.

Alimtaka IGP atoe tamko la kuvunjwa kwa vikosi kazi vyote vilivyoundwa ambavyo vimekuwa vikifanya kazi kinyume na sheria za nchi.

Mzee Kibao mwananjeshi mstaafu, alitekwa jioni ya Septemba 6 mwaka huu, maeneo ya Kibo Complex Tegeta, Dar es Salaam, na watu waliokuwa na silaha ambao waliwataka abiria kutosema lolote, kupiga picha za mnato na mjongeo wakati wakimshusha kwenye basi la Kampuni ya Tashrif akielekea nyumbani kwake Sahare mkoani Tanga.

Mwili wake ulikutwa maeneo ya Ununio, huku ukiwa na majeraha makubwa ikiwamo usoni.

**WADAIWA KUTISHIWA MAISHA**

Wakati huo huo, TLS ilitoa taarifa jana jioni kuwa imepokea kwa masikitiko taarifa ya kutishiwa maisha kwa mawakili Tito Magoti, Peter Madeleka na Onesmo Ole Ngurumwa.

Taarifa ya TLS iliyotolewa na Mwabukusi, ilisema kuwa walipokea taarifa kutoka kwa mawakili hao na kwamba vitendo hivyo ni kinyume cha Katiba.

"TLS inachukua kwa uzito usalama wa maisha ya wanachama wake wote. Wakili ana haki ya kisheria ya kuzungumza na kutoa maoni yake bila vikwazo na ana haki ya uhuru kwa kutumia haki hii katika kuelimisha jamii kuhusu haki za raia na utawala wa sheria," alisema.

"TLS inalaani vitendo vyovyote vinavyoashiria kutishia au kufifisha utendaji wa mawakili katika kazi zao kama maofisa wa mahakama na majukumu mengine waliyonayo kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Mawakili Tanganyika.

"Vitisho vyovyote kwa wakili au mawakili ni vitisho kwa muhimili wa mahakama, vitisho kwa waheshimiwa majaji na mahakimu. Kwa ustawi wa taifa letu, TLS inatoa wito kwa serikali kutoruhusu hata kidogo kwa chombo hiki muhimu na kikubwa nchini chenye jukumu mahsusi la kutafsiri sheria na kutoa haki kwa watu wote, kutishiwa."

# Madalali wamkaba mwandishi kwenye bomoabomoa Dar es Salaam

**Na Zanura Mollel**

MPIGAPICHA wa Gazeti la Nipashe, Imani Nathaniel, jana alishambuliwa na watu wanaodaiwa kuwa ni madalali wa mahakama waliokwenda kuvunja nyumba eneo la Upanga Magharibi, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana akiwa Kituo cha Polisi Selander Bridge kwa ajili ya kutoa maelezo yake, Mwandishi Imani alisema: "Ilikuwa ni majira ya saa nane mchana alipoelekea katika eneo hilo ambapo kulikuwapo na zoezi la kuhamisha watu waliokuwa wamepanga katika nyumba namba 266 barabara ya Alykhan Upanga."

Alisema alifika eneo hilo ili kuanza kutekeleza wajibu wake kama mwandishi kwa kuanza kupiga picha wakati wa kuondoa vitu vya wapangaji waliokuwa wakiishi katika nyumba hiyo.

Alisema wakati anaanza kupiga picha, ghafla alishambuliwa kwa vipigo na mabaunsa waliokuwa wameambatana na madalali wa Kampuni ya Bilo Star Debt Collectors Co. Ltd.

"Walinipiga na kuninyang'anya kifaa changu cha kazi (kamera) pamoja na kunifunga pingu katika mikono yangu. Walifuta picha zote nilizokuwa nimepiga kupitia kamera yangu.

"Baada ya muda nilifanikiwa kumwona kiongozi wao nilimweleza hali hiyo, kisha aliamuru nirejeshewe kamera, na kuachiwe huru na kunitaka niondoke katika eneo hilo mara moja.

Mwandishi aliona barua ya notisi ya kuhama eneo hilo yenye kumbukumbu Na:BSDC/DCR/09/2024/04 yenye kichwa cha barua "Notisi ya siku saba kuhama kwenye nyumba/eneo plot No, 266 iliyoko Upanga, Dar es Salaam iliyotolewa na Julitha Bartalomeo kwa niaba ya kampuni.

Barua hiyo ilionyesha kutolewa na kampuni hiyo kuwataka wapangaji katika nyumba hiyo kuondoka ndani ya siku saba kwa amri ya mteja wao aliyetambulishwa kwa majina ya Jammale Mohamed Said.

Katika barua hiyo pia ilionekana nakala kuwasilishwa kwa mkuu wa kituo cha polisi pamoja na ofisi ya serikali ya mtaa (haijataja kituo kipi cha polisi wala ofisi ya serikali ya mtaa).

Kutokana na tukio hilo, Nathanael alisema ameripoti Kituo cha Polisi Selander saa 9:33 alasiri kwa lengo la kutoa taarifa kutokana na shambulio hilo alilofanyiwa.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, akifungua pazia kuzindua kituo kipya cha polisi Lushoto, kilichojengwa kwa gharama ya Sh. milioni 400, wilayani Lushoto, mkoani Tanga jana. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Japhari Kubecha na Mkuu wa wilaya hiyo, Zephania Sumaye. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# REA kutia saini mikataba ya bil. 73/- kusambaza mitungi ya gesi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA), kesho unatarajia kutia saini mikataba sita yenye thamani ya Sh. bilioni 72.8, ukiwamo wa kusambaza mitungi ya gesi yenye ruzuku ya kilogramu sita kwa kaya za vijijini itakayopatikana kwa bei nafuu.

Kati ya fedha hizo, REA itachangia Sh.bilioni 62.75 huku Jeshi la Magereza litachangia Sh.bilioni 8.66 na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) litatoa Sh.bilioni 1.39.

Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Jadidifu na Mbadala wa REA, Mhandisi Advera Mwijage, alisema jana jijini hapa kuwa mikataba hiyo ni utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia wa mwaka 2024 hadi 2034.

Alisema Sh. bilioni 10 zitatumika katika mkataba wa kusambaza mitungi 452,445 kwa bei ya ruzuku katika mikoa yote na kila wilaya itanufaika na mitungi 3,255.

"Mitungi hii itapatikana kwa bei ya punguzo. Kwa mfano mtungi ule wa kilo sita unauzwa Sh.45,000 lakini kwa bei ya ruzuku ni Sh. 20,000," alisema.

Pia alisema Sh. bilioni 15 zimetengwa na REA kwa ajili ya kuwezesha usambazaji wa zaidi ya majiko banifu 200,000 ambayo yatauzwa kwa bei ya ruzuku.

Kadhalika, alisema REA imefikia makubaliano ya ushirikiano wa utekelezaji wa miradi ya kujenga na kusambaza mifumo ya nishati safi ya kupikia kwa magereza Sh.bilioni 35.23 zitatumika kujenga mifumo ya gesivunde 126, usimikaji wa mifumo ya gesi LPG 64, gesi asilia mmoja.

"Mkataba huu wa miaka mitatu pia utasambaza mitungi ya LPG ya kilogramu 15 ikiwa na jiko la plate mbili yapatayo 15,920 kwa watumishi wa magereza, usambazaji wa tani 865 za mkaa mbadala unaotokana na makaa ya mawe kutoka STAMICO," alisema.

Aidha, alisema mradi huo utahusisha usambazaji wa mashine za kutengeneza mkaa mbadala 61 ambapo miradi hiyo itatekelezwa magereza 129 yaliyopo Tanzania Bara.

Kuhusu mkataba na JKT, alisema Sh.bilioni 5.75 zitatumika kujenga mifumo ya bayogesi tisa, majiko 291 ya mkaa mbadala, ujenzi wa mifumo ya gesi LPG 180 na sufuria zake, ununuzi wa mkaa unaotokana na makaa ya mawe tani 110, ununuzi wa mashine 60 kutengeneza mkaa mbadala na mafunzo kwa vijana 50,000.

Alisema miradi itatekelezwa kambi za JKT 22 zilizopo mikoa 14 ya Tanzania Bara ndani ya miaka miwili.

"Wakala pia unafadhili mradi wa usambazaji wa gesi asilia, mradi unatekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa ufadhili wa REA kwa gharama ya Sh. bilioni 6.82, mradi utatekelezwa mkoani Lindi na Pwani, utakaounganisha kaya 980, kati ya hao wateja 451 wa Lindi na 529 ni wa Pwani," alisema.

# NECTA yafafanua kilichobadilika kwenye Mtihani wa Darasa la VII

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA) limetoa ufafanuzi wa kilichobadilika kwenye Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi, ulioanza jana na unakamilika leo.

Katika toleo letu la jana, tulikuwa na habari kuhusu mtihani huo ikiwa na kichwa kilichosomeka "Darasa la VII kuanza leo siku mbili za mitihani mipya 'migumu'".

Hata hivyo, katika taarifa yake jana kwa Nipashe, baraza hilo lilisema mabadiliko hayo hayalengi kufanya mtihani huo kuwa mgumu, bali ni mabadiliko ya muundo. Ofisa Habari wa NECTA, John Nchimbi, alisema kuwa kilichofanyika ni "maboresho ya Fomati ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi".

Kwa mujibu wa NECTA, jumla ya watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani huo ni 1,230,780. Kati yao, wavulana ni 564,176 sawa na asilimia 45.84 na wasichana ni 666.604 sawa na asilimia 54.16.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Ally Mohamed, alibainisha kuwa kati ya watahiniwa 1,230,780 waliosajiliwa 1,158,862 sawa na asilimia 94.16 watafanya mtihani kwa lugha ya Kiswahili na watahiniwa 71,918 sawa na asilimia 5.84 watafanya kwa lugha ya Kiingereza ambayo wamekuwa wanaitumia katika kujifunza.

**Mhariri**

# Tanzania yatajwa kuongoza kuwa na simba wengi

**Na Joseph Mwendapole**

TANZANIA imetajwa kuongoza kwa kuwa na simba wengi zaidi barani Afrika wanaofikia 17,000 na inashika nafasi ya tatu Afrika kwa kuwa na tembo 60,000 kwa mujibu wa taarifa za mwaka huu.

Ofisa Wanyamapori kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Gideon Msenya, alisema hayo jana wakati akiwasilisha mada kwenye mkutano na waandishi wa habari ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET).

Mkutano huo uliofanyika jijini Dar es Salaam ulikuwa ukijadili kuhusu hatua zinazochukuliwa na serikali katika mradi unaofadhiliwa na GIZ wa kutatua changamoto baina ya binadamu na wanyamapori kanda ya Ruvuma.

Alisema takwimu zilizopatikana mwaka huu zinaonyesha kuwa Tanzania ina chui 24,000, nyati 225,000.

Wizara hiyo, alisema kwa kushirikiana na GIZ inaendelea kutekeleza mradi huo wa kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori unaotarajiwa kukamilika mwakani.

Alisema Sh. bilioni 45.1 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto ya wanyama wakali na waharibifu nchi nzima kwa mwaka 2024/25.

"Kwa kuwa suala hili ni mtambuka wizara inatambua mchango wa wadau na itaendelea kushirikiana na wizara za kisekta na wadau wa uhifadhi katika utatuzi wa changamoto na kufanya tathmini ya mkakati na maandalizi ya mkakati mpya," alisema.

Kupitia mradi huo, alisema wizara imewapa mafunzo walimu 59 na wakulima 1,550 kuhusu mbinu za kukabiliana na uharibifu unaoweza kufanywa na wanyama hao shambani.

Alisema serikali imefanikisha kufunga uzio wa kilomita 23 unaotoa harufu mbaya hivyo kuwakinga na tembo wakulima 280, ekari 1,300 na vjiji 24.

Pia, alisema wameimarisha programu ya wilaya ya kutatua migongano na kutoa mafunzo ya kilimo bora kwa kushirikiana na Shirika la Swiss Aid na kuanzisha vikundi vya kijamii kukabiliana na hali hiyo.

Alisema wamefanikisha kuanzishwa kwa mfumo wa kidigitali wa ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za matukio ya migongano ambao unatumia simu janja na vishikwambi kukusanya taarifa na kupelekwa kwenye mfumo kwa hatua za haraka.

Mfumo huo, alisema umeshaonesha mafanikio makubwa kwenye wilaya ambazo umewekwa na kwamba mpango wa serikali ni kuhakikisha unaendelezwa na kuwekwa wilaya zote.

Alisema pamoja na mafanikio ya mradi huo migongano baina ya binadamu na wanyamapori bado inaongezeka na kwamba wilaya 41 kati ya 91 zimebainika kuathirika zaidi na changamoto hiyo.

Alisema Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), imechapisha mwongozo wa utafiti nchini unaoainisha pia migongano kama moja ya maeneo yanayohitaji tafiti zaidi na kwamba tafiti zinaendelea maeneo mbalimbali ya nchi zikiwahusisha watafiti mbalimbali.

HABARI KITAIFA

# 195 watibiwa fistula bila malipo

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

KINAMAMA 195 waliokuwa wanasumbuliwa na ugonjwa wa fistula ya uzazi na magonjwa mengine ya wanawake mkoani Lindi, wamepatiwa matibabu bila malipo tangu kuanza kwa ushirikiano kati ya CCBRT, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi (Sokoine) na Shirika la Equinor Tanzania mwaka 2019.

Kwa mwaka huu, kambi ya matibabu ya fistula imefanyika tena mkoani Lindi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi (Sokoine) kuanzia Septemba 9 hadi 13, 2024, ambapo jumla ya wanawake 10 wenye ugonjwa huo mkoani Lindi wamepatiwa matibabu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika hospitali hiyo jana, Meneja wa Miradi wa hospitali ya CCBRT, Yohana Kasawala, alisema "CCBRT inatoa shukrani zake za kwa wadau wake wote, ikiwamo Equinor Tanzania, na kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutushika mkono na hivyo kuwezesha kuwafikia Watanzania wenzetu wenye mahitaji makubwa ya kiafya.

"Kwa mfano, maisha ya wanawake walioathirika na ugonjwa wa fistula yameboreshwa kutokana na matibabu katika Hospitali ya CCBRT na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi - Sokoine."

Alimshukuru Dk. Naomi Makota, Msimamizi wa Miradi ya Jamii kutoka Equinor kwa kushiriki katika kambi inayoendelea mjini Lindi.

Kuhusu mafunzo ya wanawake waliokuwa wanaishi na fistula, Kasawala alisema kuwa mara nyingi wanawake hao hufika hospitalini kwake wakiwa wamekata tamaa na sononа kutokana na kutengwa na jamii zao na wakati mwingine kupoteza wenza na watoto wao.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Upasuaji wa Fistula, Peter Majinge, alisema kuwa hadi kufikia jana, jumla ya wanawake 20 walifika katika Hospitali ya Sokoine na baada ya uchunguzi, wanawake 10 wamegundulika kuwa na fistula ya uzazi, hivyo wanaendelea kupatiwa matibabu ya upasuaji.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Dk. Kheri Kagya, aliishukuru CCBRT na wadau wake Equinor kwa kuendelea kuwajengea uwezo wataalamu wake wa afya ya uzazi mkoani Lindi ili mara baada ya kumalizika kwa mradi huo, waweze kutoa huduma hiyo hospitalini Sokoine kwa kuwa hilo ndilo lengo la mradi tofauti na ilivyo kwa sasa ambapo wagonjwa hulazimika kusafiri umbali mrefu kwenda CCBRT Dar es Salaam kwa ajili ya matibabu.

Saada Hassan (50) kutoka Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi ni mnufaika wa mradi huo wa matibabu ya fistula. Alikutwa wodini katika Hospitali ya Sokoine, akisema:

"Mwezi uliopita nilisikia tangazo redioni likieleza juu ya ugonjwa huu, baada ya kusikiliza vizuri nilibaini kuwa ndio ugonjwa unaonisumbua, nikachukua namba ya simu waliyotangaza redioni, nikaipiga nikaelekezwa kuwa wataalamu wa matibabu ya fistula toka Dar Salaam watakuwa hapa kwetu Lindi, sikuamini hadi juzi nilipopigiwa simu na kutumiwa nauli ya kuja hospitalini hapa.

"Nimeteseka na fistula ya uzazi kwa takribani miaka 10, baada ya kujifungua mtoto wangu wa mwisho. Kipindi hiki kilikuwa na changamoto kubwa sana, si tu kimaisha bali pia kiroho na kijamii."

# Serikali haitavumilia udanganyifu, kuchezea mifumo maalum ya afya

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema haitavumilia udanganyifu na uchezeaji wa mifumo ya huduma za matibabu kupitia bima ya afya itakayosimamiwa na mfuko maalum, kuelekea huduma ya Afya kwa Wote.

Waziri wa Afya, Jenista Mahagama, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kufanya ziara katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) na kwamba lengo ni kuboresha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na ufanye majukumu yake ipasavyo.

"Kwa kweli tutakuwa wakali na mimi nitakuwa mkali kabisa, kusimamia na kuhakikisha fedha zitazotumika kusimamia matibabu kutoka katika mfuko zinatumika kwa wakati, mahala sahihi. NHIF tumeona hapo katikati ulivyoyumba, kipindi hiki cha mpito tunaiboresha kwanza.

"Hatuko tayari kumvumilia mtu ambaye atachezea mifumo yetu. Huko nyuma kumekuwa na udanganyifu na hatutakuwa tayari. Afya ni usalama na ikiwa bora na yenye ustawi ni usalama. Lazima tuwe na mfumo wa kutrack (kufuatilia) tangu mgonjwa anapokelewa, anaanza huduma hadi anamaliza," alisema.

"Mfumo wa Afya kwa Wote unalenga kuwafikia wananchi wote, tunaweza kuwa na tiba nzuri sana na isipowafikia wanyonge inakuwa haina maana. Tunalenga pia kuzitambua hospitali zinazofanya vyema kwenye utoaji huduma, lakini baada ya kuwezeshwa katika ubobezi," aliongeza.

Pia alisema JKCI ni mfano wa kuigwa kutokana na kutoka matibabu bobezi na ya kibingwa kwa Kanda ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini huku ikipokea wageni wakiwamo watalii.

"Nilichoona ni bado huduma za matibabu ni kubwa na lengo ni huduma kumfikia kila mmoja. Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote ni maono ya Rais nami nitafanyia kazi hilo, bima hii iwezeshe kila mmoja kufikika. Tunamalizia kanuni ili wananchi waanze kutumia Afya kwa Wote," alisema Mhagama.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema uwekezaji uliofanywa na serikali umeongeza upatikanaji wa huduma bora na za kibingwa na kwamba kupitia mpango wa Tiba Mkoba ya Rais Samia, imewezesha kuwafikia wananchi zaidi ya 17,000 nchi nzima.

"Mpango huo uliowezeshwa na Rais umesaidia kuwapatia wagonjwa wenye matatizo na hapa JKCI tunafanya operesheni nne hadi tano kwa siku. Kwa wagonjwa wa nje (OPD), tunayaona takribani wagonjwa 500 kwa siku," alisema Dk. Kisenge.



Fundi wa Kampuni ya Sinohydro, akiendelea na maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (BRT), katika Barabara ya Bibi Titi Mohamed, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CCM kutumia wapinzani kupata siri maandalizi uchaguzi mitaa

**Na Salome Kitomari, Aliyekuwa** KITETO

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, amewataka wana CCM kutowapuuza wapinzani wanaohamia kwenye chama hicho. Badala yake amewataka wawatumie kupata mikakati iliyokuwapo kuelekea uchaguzi.

Akizungumza na wananchi katika Kata ya Engusero, Kiteto mkoani Manyara, alisema katika ziara yake kwenye mikoa ya Arusha na Manyara, idadi ya wanachama wa upinzani na viongozi wao wanaohamia CCM ni kubwa na inazidi kuongezeka.

"Tufanye nao kazi watatusaidia. Kama Katibu wa Chama cha Wananchi (CUF) wilaya anaondoka aliacha mikakati ya chama huko (kwenye vyama), maana yake atakusaidia chama kushinda uchaguzi, hivyo tuwatumie wanachama na viongozi wao ili tupate siri za upande mwingine (upinzani)," alisema Makalla.

Pia alisema umaarufu wa vyama vya upinzani umepungua kutokana na kuwa vya matukio pekee, huku wanachama wao wakikimbilia CCM hali inayoonesha ndicho chama cha matumaini.

Kwa mujibu wa Makalla, CCM ni chama kinachoaminika na chenye wajibu wa maisha ya Watanzania, hivyo kitaendelea kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Aidha, Makalla aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Wakazi la Kijiji kuanzia Oktoba 11 hadi 20, mwaka huu, ili wapate sifa ya kuchagua Novemba 27, mwaka huu, na kuwa na uhakika wa ushindi wa CCM.

"Ninawaomba tutumie nafasi hiyo tujiandikishe ili kuipa CCM ushindi. Ninafurahi katika vijiji 66 na mitaa 20 tunataka yote iende CCM," alisema.

Pia alisema CCM haitaki watu kuteuana kwa kujuana au urafiki bali anayekubalika na kuaminiwa na wananchi, na kwamba chama hicho hakipo tayari kupewa mgombea wa kumsafisha kwa dodoki.

"Zipo sababu nyingi za kuwaomba mtuchague, tumetekeleza Ilani ya uchaguzi, nilivyofika Kiteto leo sio ya miaka 1998, kuna mtu anaweza kusema Kiteto haina maendeleo, akikwambia hivyo jua ana matatizo ya akili au ni mgeni," alisema.

Kwa mujibu wa Makalla, CCM inawajibu na dhamana ya kuwaletea wananchi maendeleo, hivyo wananchi wanapaswa kukiamini na kuendelea kukiweka madarakani.

Alisema Barabara ya Kiteto hadi Njiapanda NARCO serikali imaishughulikia ili ijengwe kwa kiwango cha lami.

Pia alilaani matukio la ulawiti baada ya tukio la mama na mwanawe kulawitiwa na kuuawa, na kuwataka viongozi wa dini kukemea.

Aidha, aliwataka wananchi kutowaamini waganga kwa kuwa ni waongo na kusababisha matatizo kwenye jamii kwa kucheza na akili za watu.

"Imani za kishirikina zisitupelekee kutenda maovu, Jumuiya ya Wazazi, Jumuiya ya Wanawake kemeeni na kuendelea na kampeni ya kupiga vita matukio haya," alisema.

Kiongozi huyo alipokea kero 85 za elimu, wajasiriamali kudhulumiwa Sh. milioni 100, eneo la malisho kubadilishwa matumizi, wanyamapori, uchaguzi wa mbunge na diwani urudishwe kwa wanachama wote, shule yenye walimu wa kiume pekee, ubovu wa barabara vijijini.

Zingine ni kukosekana kwa maneneo ya malisho, malumbano kati ya wakulima na wafugaji, ahadi ya mifuko 100 ya aliyekuwa Katibu Mkuu katika Zahanati ya Chapakazi na nyumba ya watumishi.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utunzaji mazingira ni jukumu la kila mmoja

**JUZI** wakati Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akifunga mkutano maalum wa viongozi na wadau wa mazingira ulioitishwa ili kujadili mwenendo wa mazingira nchini, aliagiza kuwa suala la uhifadhi wa mazingira liwe ajenda ya kitaifa na jukumu la kila mmoja kuanzia ngazi ya familia mpaka taifa.

Uchafuzi wa mazingira umeleta athari kubwa katika mabadiliko ya tabianchi, hali iliyosababisha baadhi ya maeneo kukosa mvua na kuleta upungufu wa chakula.

Athari za mabadiliko ya tabianchi zimeshuhudiwa katika baadhi ya maeneo ambako mvua imenyesha kupita kiwango na watu kukosa makazi na hata kusababisha vifo.

Waziri Mkuu akielezea umuhimu wa kuhifadhi mazingira alitaka uanzie katika ngazi ya familia na kupanua wigo hadi kwa wadau mbalimbali.

Watu muhimu na wanaosikilizwa katika jamii ni viongozi wa dini ambao Waziri Mkuu alisema wanayo nafasi kubwa na kuwataka iwe ajenda maalum katika ofisi za umma, za binafsi au kwenye taasisi.

Umuhimu wa jamii kushiriki katika uhifadhi mazingira ni kuunga mkono juhudi za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kuendelea kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Aidha, jitihada ambazo Rais Samia amezichukua ili kuhakikisha suala la nishati safi linakubalika ni kukataa kukata miti na kuhamasisha kuhusu nishati safi ya kupikia.

Rais Samia amekuwa kinara wa nishati na alienda nchini Ufaransa kuhutubia kuhusu nishati safi na yeye akiwa ni Mwenyekiti mwenza wa mkutano huo, jambo ambalo ni ni fahari kwa nchi ya Tanzania.

Wajasiriamali wamepewa fursa kuanzisha biashara ya kuuza mitungi na majiko ya gesi hadi kwenye ngazi ya vijiji ili nishati hiyo iweze kupatikana kwa urahisi hali ambayo itaweka ukomo wa matumizi ya mkaa na kuni nchini.

Pia, serikali imechukua hatua za kisera na kimkakati ili kuleta matokeo chanya zikiwamo za kuandaliwa kwa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; kutungwa kwa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2014; kuandaa na kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2022 hadi 2032; kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2021 hadi 2026; na kutungwa kwa Kanuni na Miongozo inayohusu masuala ya Mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Wizara inayosimamia mazingira imetakiwa ishirikiane kwa karibu na wizara za kisekta kuhakikisha maadhimisho mbalimbali ya kitaifa yanayogusa masuala ya mazingira yanatumika kikamilifu kuwezesha jamii kupata uelewa na kuweka alama za kudumu na matokeo yanayopimika kuhusu utunzaji mazingira ikiwamo Siku ya Upandaji Miti, Siku ya Hali ya Hewa, Siku ya Maji, Siku ya ardhi Oevu, Siku ya Mazingira na Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni.

Uhamasishaji kuhusu utunzaji wa mazingira, Waziri Mkuu amezitaka ofisi za mikoa na wilaya, zisimamie suala hilo na kusisitiza kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria na kanuni za mazingira na ikibidi watumie mitandao ya kijamii kusambaza elimu hiyo.

Hiyo itasaidia kuongezeka kwa ufahamu miongoni mwa jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na kutasaidia kupunguza uharibifu na kuimarisha usimamizi wa mazingira. Aidha, elimu ijumuishe matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira ikiwamo matumizi bora ya ardhi, maji na nishati ili kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinabaki kuwa za kudumu kwa vizazi vijavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Tupunguze kulewa pombe jamani, inaua watu milioni 2.6 kila mwaka

Na Sabato Kasika

**SHIRIKA** la Afya Duniani (WHO), linasema kuwa watu milioni 2.6 hufariki dunia kutokana na unywaji pombe kila mwaka duniani na kwamba unywaji huo huongeza uwezekano wa kupata magonjwa hatari kama vile magonjwa ya moyo, saratani ya ini na afya mbaya ya akili.

Haya yamo katika ripoti mpya iliyotolewa na Tume ya Unywaji Pombe, Afya na Huduma kwa Waathirika wa Dawa za Kulevya, ambayo ilitolewa na shirika hilo na kukaririwa na vyombo vya habari, Juni mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, inakadiriwa watu milioni 400 wanaishi na pombe na dawa nyingine za kisaikolojia na kwamba, kati ya idadi hiyo, watu milioni 209 wanategemea kunywa pombe ili kuishi.

Shirika hilo linasema unywaji pombe ni hatari kwa afya za watu na husababisha madhara mengi kwa wale wanaokunywa pombe zaidi na kufafanua kuwa ni lazima kupunguza unywaji pombe kwa lengo la kuboresha afya na ustawi wa jamii.

Aidha, nchi za bara la Ulaya ndizo zinazotajwa na taarifa hiyo kuwa zinaongoza kwa unywaji wa vileo na kwamba inakadiriwa kuwa wastani wa pombe anayokunywa mnywaji kila mwaka ni lita 9.2.

Nikirejea kwenye hoja yangu ni kwamba, kwa kuwa nchi za bara la Ulaya ndizo zinazotajwa kuongoza kwa unywaji, lakini hatuna budi kujifunza jambo kutoka kwa hao wenzetu ili kuepuka tatizo.

Ikumbukwe kuwa Tanzania ni nchi ya tatu kwa matumizi ya pombe barani Afrika ikiongozwa na Uganda. Hayo ni kwa mujibu wa aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

Waziri huyo amewahi kusema hayo katika moja ya hotuba zake na kuwataka Watanzania kupunguza matumizi ya pombe, kwa kuwa imekuwa sababu ya kuongezeka magonjwa yasiyoambukiza,

Anakariri takwimu za WHO kuwa Tanzania watu wa kuanzia umri wa miaka 15 na kuendelea, kwa mwaka wanakunywa lita 10.4 za pombe, na kuongeza kuwa kiasi kinachonywewa nchi nzima, kikagawanywa kwa idadi ya Watanzania wa miaka 15 na kuendelea kila mmoja sawasawa, kwa mwezi mmoja lita moja, kwa mwaka ni lita 10.4.

Pia, inaelezwa kuwa chanzo kikuu cha ajali za barabarani hususan kwa waendesha bodaboda ni makosa ya kibinadamu ikiwa ni pamoja na ulevi na uzembe ambao huchangia kwa asilimia 76 ya ajali zote nchini.

Ushahidi huo unaotolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, kuhusu madhara ya unywaji pombe, unatosha kutufanya Watanzania kuwa makini dhidi ya ulevi wa kupindukia.

Kila mmoja akichukua hatua sahihi, tutakuwa salama dhidi ya magonjwa yatokanayo na ulevi. Pia, tutakuwa salama dhidi ya ajali za barabarani. Hivyo, ni muhimu kubadili mfumo wa maisha, ili kuwa salama zaidi.

Tukumbuke kuwa kupunguza unywaji wa pombe, kutasaidia kulinda afya. Pia kupunguza unywaji pombe kutasaidia kuepusha ajali za barabarani zinazoua na kuacha wengine na ulemavu.

Ingawa kuna jitihada zinazofanywa na serikali za kukabiliana na ulevi kupundukia, ikiwamo kuondoa pombe za viroba zilizokuwa zikinunuliwa kwa bei nafuu na madereva wa bodaboda, wauzaji pombe nao wamekuja na mbinu mpya na kusababisha madereva hao waendelee kuwa walevi kupindukia, kana kwamba hakuna tahadhari kwao.

Kwa mfano, baadhi ya wamiliki wa vibanda vya biashara na hata maduka ya bidhaa za kawaida mjini Dar es Salaam, wanauza pombe kwa vipimo tofauti kulingana na fedha alionayo mnunuzi.

Wanatumia vikopo vidogo kupimia pombe vikiwamo vya kuanzia shilingi 200 hadi 500. Baadhi ya madereva wa bodaboda, hukesha katika vibanda au maduka hayo ambayo huwa wazi muda wote wakinywa.

Madereva hao ndio ambao hutoka hapo wakiwa wamelewa na kwenda kubeba abiria, matokeo yake ni kusababisha ajali ambazo wakati mwingine wenyewe na abiria wao huumia au kupoteza maisha.

Ninadhani ipo haja ya kubadilika na kutoendekeza ulevi kupindukia. Hebu tujitafakari.

## HABARI KITAIFA

# Wizara ya Afya kuboresha huduma mtengamao

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Afya, imeahidi kuendelea kuboresha huduma za mtengamao kwa Watanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Huduma za mtengamao ni tiba ya maradhi na majeraha ya muda mrefu na wagonjwa wa muda mrefu kurejeshwa kwenye hali zao za kawaida ikiwamo huduma ya saikolojia.

Mkurugenzi wa Tiba Wizara ya Afya, Dk. Hamadi Nyembea, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kongamano la pili la utengamao.

Kongamano hilo lililoandaliwa na Asasi ya Rehab Health kwa kushirikisha wadau mbalimbali, litafanyika Septemba 18 hadi 20, mwaka huu na Waziri wa Afya, Jenista Mhagama.

Alisema kama ilivyo kaulimbiu ya kongamano hilo, 'Kuendeleza ajenda ya utengamao wa afya nchini. Kuimarisha mifumo ya afya', inalenga kuwakutanisha pamoja wadau wa sekta ya afya kujadili na kuweka mikakati ya kuboresha huduma hizo.

"Serikali imekuwa ikiweka msisitizo mkubwa kwenye kuimarisha huduma za afya nchini hususani wanawake, vijana, wenye ualemavu na watoto bila kujali mazingira au hali ya uchumi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Rehab Healh, Ramla Shirima, alisema kongamano hilo litahusisha pia wakufunzi kutoka nje ya nchi, wadau wa afya, watunga sera na sekta binafsi na serikali.

"Kutakuwa na mijadala maalum ya jinsi ya kuongeza huduma za mtengamao vijiji, kuimarisha uhusiano wa sekta binafsi na serikali na kuwa na sera rafiki.

"Tunawakaribisha wale wanaonufaika na huduma za afya nchini ambao wadau wakuu katika kujadili pamoja kuhusu huduma za mtengamao," alisema Shirima.

Mratibu wa Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani, Wakili Deus Sokoni, alisema Jeshi la Polisi ni mdau namba moja wa afya katika kuzingatia na kuokoa maisha na mali za watumiaji wa barabara.

Alisema wajibu wa msingi ni kutoa elimu ya usalama barabarani, kutoa takwimu zinazosomana na Wizara ya Afya na wadau wengine nchini.

"Kwenye kongamano hili tutatoa elimu ya usalama barabarani na namna tunavyoshirikiana kwa karibu na sekta afya na wadau wengine ndani na nje ya nchi," alisema.



Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa kivipimo Ilala, Muhono Nashon (kushoto), akikabidhi Kichapishi kwa Ofisa Mnadhimu wa Mkoa wa Kipolisi Ilala, ACP Mohammed Makusi, wakati wakala huo, ulipokabidhi vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa jeshi hilo, jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: WMA**

# WMA yaipiga jeki Polisi vifaa TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Vipimo (WMA) umelikabidhi Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Kipolisi Ilala, Dar es Salaam, vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ikiwa sehemu ya kulisaidia kupambana na uhalifu wa aina mbalimbali ikiwamo udanganyifu katika mizani na vipimo.

Akikabidhi vifaa hivyo jana katika makao makuu ya polisi, Dar es salaam kwa niaba wa mtendaji Mkuu wa WMA, Meneja wa Vipimo Mkoa wa Ilala, Muhono Nashon, alisema msaada huo ni kutokana na ushirikiano wa muda mrefu katika masuala ya kazi baina ya WMA na Jeshi la Polisi hususani katika masuala ya jinai, ulinzi na usalama kwa maeneo mbalimbali ya ukaguzi.

Muhono alibainisha kuwa ushirikiano huo baina ya WMA na Polisi umekuwa na tija kutokana na jeshi hilo kudumisha hali ya amani na usalama kwa watumishi wa WMA na wananchi kwa ujumla katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Pia alisema WMA imekabidhi vifaa hivyo ili kuunga mkono matumizi ya TEHAMA kwa taasisi mbalimbali za serikali likiwamo Jeshi la Polisi.

"Vifaa hivi vitatumiwa na Jeshi letu katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali na ni matumaini yetu kuwa vitaongeza ufanisi katika utendaji wake," alisema Nashon.

**Muhono alibainisha kuwa ushirikiano huo baina ya WMA na Polisi umekuwa na tija kutokana na jeshi hilo kudumisha hali ya amani na usalama kwa watumishi wa WMA na wananchi kwa ujumla katika shughuli mbalimbali...**

Kamishna Msaidizi wa Polisi na Ofisa Mnadhimu wa Mkoa wa Kipolisi Ilala, Kamishna msaidizi (ACP) Mohammed Makusi, aliishukuru WMA kwa msaada huo na kusisitiza kuwa jeshi hilo litaendelea kutumia TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yake ili kuwahudumia wananchi kwa ufanisi zaidi.

"Vifaa hivi vimekuja wakati muafaka tukielekea katika Wiki ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Jeshi la Polisi Tanzania ambayo yatafikia kilele chake Septemba 27, 2024," alisema.


ACP Makusi alisema kaulinbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ni 'Huduma Bora za Kipolisi zitapatikana kwa Kubadili fikra, usimamizi wa sheria na matumizi ya TEHAMA'.

"WMA mmetuunga mkono katika TEHAMA, hivyo tunawashukuru kwa hiki mlichotupatia ambacho kitasaidia kuboresha huduma zetu," alisisitiza Makusi.

WMA imekuwa na utaratibu endelevu wa kuimarisha ushirikiano na wadau na taasisi mbalimbali za serikali na binafsi kwa kutoa elimu ya matumizi sahihi ya vipimo, ushauri wa kitaalamu, semina elekezi na uwezeshaji kwa baadhi ya taasisi.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed






Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Janeth Shango (wa tatu kushoto), akikabidhi sehemu ya msaada wa vifaa tiba kwa Meneja Mkuu wa Shirika la Mzinga na Mkuu wa Kikosi cha Jeshi Mazao, Brigedia Jenerali Seif Athumani Hamis, mjini Morogoro jana. Vifaa hivyo ni pamoja na vitanda, magodoro na viti mwendo 10. Wengine ni Meneja Uhusiano wa benki hiyo Kanda ya Kati, Christabel Hiza (kushoto), Meneja wa NMB Tawi la SUA, Josephat Mwaipaja (wa pili kushoto), Naibu Kamanda wa Kikosi cha Jeshi Mazao na Mwanasheria wa Shirika la Mzinga, Kanali Undule Kabunda (kulia) na (wa pili kulia) ni Mganga Mkuu wa Hospitali ya Shirika hilo, Luteni Kanali Dk. Fredrick Gady Maeda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mashirika 8 yapaza sauti ulinzi, haki za wasichana

**Na Elizabeth Zaya**

MASHIRIKA ya kutetea haki za wasichana Tanzania, yamewaomba wadau pamoja na serikali kuweka sera na sheria zitakazoimarisha ulinzi wa kundi hilo, kuendeleza haki zao za msingi ikiwamo kupewa nafasi za uongozi.

Mashirika hayo ikiwamo la Msichana Initiative, TAI, GLAMI, Flaviana Matata Foundation, CSema, Young Strong Mothers Foundation na WoteSawa, yamesema bado baadhi ya jamii zinaendeleza mila kandamizi ambazo zinaminya baadhi ya haki za msingi za wasichana.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kutoka Shirika la Msichana Initiative, Sara Bedah, alisema bado wasichana wanawekwa nyuma zaidi kwenye masuala mengi ikiwamo ya uongozi na nyanja mbalimbali kuanzia nyumbani, shuleni na kwenye jamii kwa ujumla.

"Kwa hiyo katika kuadhimisha siku ya mtoto wa kike mwaka huu, wadau wa haki za wasichana kutoka katika mashirika saba nguvu kubwa kwa sasa ni juu ya elimu ya wasichana na ushiriki wao katika michakato ya kisiasa kuhakikisha kwamba unawekwa msingi wa viongozi wa kike wa baadaye nchini," alisema Sara.

**"Hata hivyo, inaonekana kuwa, wasichana wako nyuma zaidi kwenye masuala ya michakato ya uongozi katika nyanja mbalimbali. Mfano, utakuta kama ni nyumbani mtoto wa kiume anashirikishwa na kutoa mawazo yake kuhusu masuala mbalimbali ya kimaendeleo ...**

"Tafiti zinaonyesha kuwa asilimia 44.4 ya wanafunzi wa sekondari hawaelewi maana ya demokrasia huku asilimia 85.5 hawajawahi kushiriki wala kushirikishwa katika vikao rasmi vya shule vinavyofanya uamuzi.

"Pia, asilimia 68.9 ya wanafunzi hawajawahi kugombea au kuonesha nia ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi ngazi ya shule huku asilimia 44 hawashiriki katika chaguzi za uongozi wa wanafunzi."

Alisema kaulimbiu ya mwaka huu katika siku ya mtoto inasema wasichana na uongozi pamoja na kutumia fursa ya teknolojia za kidijitali na kwamba kipaumbele zaidi katika maadhimisho hayo mwaka huu wamewekeza katika kuwawezesha wanawake vijana kujitokeza nafasi za uongozi katika sekta mbalimbali.

"Hata hivyo, inaonekana kuwa, wasichana wako nyuma zaidi kwenye masuala ya michakato ya uongozi katika nyanja mbalimbali. Mfano, utakuta kama ni nyumbani mtoto wa kiume anashirikishwa na kutoa mawazo yake kuhusu masuala mbalimbali ya kimaendeleo nyumbani, lakini mtoto wa kike hapewi nafasi hiyo," alisema Sara.

"Ndio maana ajenda ya msichana mwaka huu itazingatia umuhimu wa wasichana na uongozi katika kuwawezesha wasichana kufikia malengo yao ya uongozi ili kufungua milango ya fursa kwa wasichana kujifunza, kujieleza na kusimamia mabadiliko chanya katika jamii zao."

# Mume adaiwa kumuua mke kwa kumchinja

**Na Steven William,** MUHEZA

MKAZI wa Kijiji cha Perani, Kata ya Mwakijembe wilayani Mkinga, mkoani Tanga, SAUMU Ngome (19) ameuawa kikatili na anayedaiwa kuwa mume wake Sarah Nzuga kwa kutenganishwa kichwa na kiwiliwili kwa kisu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Almachius Mchunguzi, alisema mauaji hayo yametokana na wivu wa kimapenzi huku kila mmoja akimtuhumu mwenzake kutoka nje ya ndoa.

Alisema kuwa tayari Jeshi la Polisi limemtia mbaroni mume wa marehemu kwa tuhuma za mauaji hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Gilbert Kalima, alisema kuwa kifo cha mwanamke huyo kimewapa simanzi wananchi kwa kuwa ni cha kikatili.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwakijembe, Juma Ngendage, alisema kuwa kutokana na kitendo hicho cha kinyama ameomba hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya mtuhumiwa.

# Wateja Benki Absa wapata fursa kujishindia gari

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Absa Tanzania imezindua kampeni ya "Spend & Win," ambayo ni promosheni ya kusisimua inayolenga kuhimiza matumizi ya njia za kidijitali za kibenki huku ikiwapa wateja fursa ya kushinda gari mpya aina ya Subaru Forester 2014 kila mwezi kwa miezi mitatu ijayo. Kampeni hiyo inasisitiza dhamira ya benki katika kuendeleza ujumuishaji wa kifedha na inalingana na lengo lake la "Kuwawezesha Waafrika wa kesho, pamoja, hatua moja baada ya nyingine" na ahadi yake ya chapa "Stori yako ni thamani."

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya Absa Tanzania, Bernard Tesha, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Obedi Laiser, alisisitiza lengo la kampeni hiyo la kukuza matumizi ya teknolojia za kidigitali nchini kote.

"Tumewekeza sana katika mabadiliko ya kidijitali ili kuhakikisha tunakidhi mahitaji ya wateja wetu yanayobadilika huku tukiiunga mkono ajenda ya serikali ya kuongeza ujumuishaji wa kifedha," alisema Tesha. "Kampeni ya 'Spend & Win' imeundwa kuhimiza Watanzania wengi zaidi kutumia suluhisho za kibenki za kidijitali, kama vile kadi zetu za debit na credit, ambazo hutoa usalama, urahisi, na upatikanaji wa huduma mbalimbali za kibenki."

Kampeni hiyo, iliyoanza Septemba 10 hadi Desemba 10, mwaka huu, itamfanya mteja mmoja mwenye bahati kila mwezi kushinda Subaru Forester 2014. Forester, inayojulikana kwa kuwa moja ya SUV zinazouzwa zaidi za Subaru na kupigiwa kura kuwa moja ya magari salama zaidi sokoni, inalingana na dhamira ya Absa ya kuhakikisha usalama wa wateja wake. Tesha alihusisha usalama wa gari hilo maarufu na usalama wa miamala ya kadi za Absa.

Mchakato wa kampeni ni rahisi - mteja yeyote wa Benki ya Absa Tanzania anayefanya miamala kwa kutumia kadi yake ya debit au credit moja kwa moja anastahiki kuingia kwenye droo ya bahati nasibu. Wateja watakaokidhi kigezo cha miamala 20 ya kadi, yenye thamani ya jumla ya angalau Shilingi milioni tano ndani ya kipindi cha kampeni, watapata tiketi za droo ya kila mwezi. Aidha, wateja wanaotumia majukwaa ya kidijitali ya benki ya Absa watapata tiketi za bonasi.

Ndabu Swere, Mkuu wa Kitengo cha Benki cha Wateja Binafsi, alifafanua kuhusu masharti ya kampeni hiyo: "Tunataka kampeni hii iwe shirikishi na yenye matokeo chanya. Wateja waliopo pamoja na wateja wapya wanakaribishwa kushiriki. Kadri wanavyofanya miamala mingi, ndivyo nafasi zao za kushinda zinavyoongezeka," alisema Ndabu.

"Miamala ya kibenki ya kidijitali kupitia majukwaa kama vile Absa Mobile Banking, Internet Banking na Hello Money pia inawapa wateja tiketi za ziada za droo, kuhakikisha kwamba wale wanaotumia suluhisho za kidijitali wanapata nafasi kubwa zaidi ya kushinda."

Kampeni ya "Spend & Win" pia inaunga mkono lengo la Absa la kupanua ujumuishaji wa kifedha nchini Tanzania kwa kuhimiza wateja kuachana na njia za kibenki za kiasili na kuhamia kwenye miamala ya kidijitali. Matumizi ya teknolojia za kidigitali yanatoa urahisi na pia husaidia kupunguza miamala inayotegemea fedha taslimu, jambo ambalo ni muhimu kwa jitihada za serikali za kukuza ujumuishaji wa kifedha.

"Kampeni inyokwenda kwa jina la, 'Kushinda gari kunaweza kubadilisha hadithi yako,' kinatokana na ahadi yetu ya chapa 'Stori yako ina thamani.' Katika Absa, tunataka kuwa sehemu ya safari ya wateja wetu, tukiwasaidia kufikia malengo na ndoto zao, hatua kwa hatua," aliongeza Tesha.



# Matumizi ya umeme yawakutanisha wataalamu nchi 13

**Na Godfrey Mushi**, ARUSHA

WATAALAMU wa nishati ya umeme kutoka nchi 13 za Mashariki mwa Afrika wamekutana jijini Arusha kujadili mahitaji ya umeme katika kipindi cha miaka 50 ijayo na namna ya kuvitumia vyanzo vipya vya nishati hiyo ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Msimamizi wa mafunzo hayo Kanda ya Afrika, Dennis Mwalongo, alisema wataalamu hao kutoka nchi wanachama wa Dimbwi la Nishati Afrika Mashariki (EAPP), watajadili kwa wiki mbili namna ya upatikanaji wa nishati ya umeme kupitia vyanzo mbalimbali vya asili ikiwamo joto la ardhi.

Mwalongo alisema mafunzo hayo yameandaliwa na Shirika la Kimataifa la Nishati za Atomic pamoja na Dimbwi la Nishati la Afrika Mashariki (EAPP) na watajadili pia makadirio ya mahitaji ya umeme katika kipindi cha miaka 50 ijayo kwa kutumia takwimu za idadi ya watu.

"Wataalamu hawa wamekutana kwa ajili ya kujadili mahitaji ya umeme kwa Kanda ya Mashariki katika kipindi cha miaka 50 ijayo ukizingatia kwamba matumizi ya umeme katika kanda ya Afrika Mashariki yamekuwa makubwa kwa sababu watu wanaongezeka."

Alizitaja baadhi ya nchi wanachama watakaoshiriki kuwa ni Ethiopia na Kenya, ambazo zimepiga hatua kubwa katika vyanzo vikubwa vya nishati ya umeme na kufikia hatua ya kuuza umeme kwa nchi nyingine hivyo wataalamu hao watajadili na kuibuka na majibu ya jinsi gani nchi zingine wanachama zinaweza kuwa na vyanzo vya nishati.

**"Tanzania imepiga hatua kubwa katika suala la uzalishaji wa nishati ya umeme kutoka vyanzo asili ikiwamo gesi na tunaimani katika kipindi cha mbeleni itakuwa na umeme mwingi wa**

Naye Katibu Mkuu wa Shirika la EAPP, James Wahogo, alisema nchi wanachama zinauzalishaji mkubwa wa umeme na wataangalia namna ya nchi hizo ziweze kupeana umeme kwa kuuziana.

"Tanzania imepiga hatua kubwa katika suala la uzalishaji wa nishati ya umeme kutoka vyanzo asili ikiwamo gesi na tunaimani katika kipindi cha mbeleni itakuwa na umeme mwingi wa ziada na kuziuzia nchi za jirani," alisema.

Wahogo alizitaja nchi hizo zinazounda umoja wa EAPP kuwa ni Burundi, Comoro, DRC Congo, Djibouti, Misri, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Libya, Madagascar, Malawi, Rwanda, Shelisheli, Sudan Kusini, Sudan, Tanzania, Uganda na Zambia.

Mmoja ya washiriki kutoka TANESCO Idara ya Mipango nchini Tanzania, Mhandisi Mwandamizi Alex Heruka, alisema mafunzo hayo ya kitaalamu yanalenga kufanya makadirio ya matumizi ya umeme kupitia vyanzo mbalimbali vya nishati.

"Ushiriki wetu katika mafunzo haya utasaidia kujifunza makadirio kupitia vyanzo mbalimbali vya kufua umeme kama maji, gesi, makaa ya mawe, jua na upepo na hii itasaidia kuepuka athari za mabadiliko ya tabia ya nchi," alisema.

Alisema kwa sasa Tanzania imekamilisha kuunganisha mifumo ya umeme kwa kujenga laini za umeme kwenda nchi ya Zambia na ipo katika hatua ya upembuzi akinifu katika nchi za Zambia, Uganda, DRC Congo, Malawi, Rwanda na Burundi ili waweze kuziuzia.



Meneja Miradi wa CCBRT, Yohana Kasawala (fulana bluu), akifafanua jambo kwa timu ya wataalamu wa matibabu ya fistula kutoka Hospitali ya CCBRT, wakati wa kambi ya matibabu bure ya ugonjwa huo, inayoendelea katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi Sokoine jana, kwa udhamini wa Shirika la Equinor Tanzania. Kutoka kulia ni Meneja Mawasiliano wa Hospitali ya CCBRT, Abdul Kajumulo, Mtaalamu wa Dawa za Usingizi, Stanley Mapunda, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Fistula, Peter Majinge, Muuguzi Theodora Kawonga, Mtaalamu wa viti mwendo, Michael Shem na Muuguzi wa CCBRT, Editha Kimega. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Prof.Kitila: Serikali haitokuwa kikwazo kwa asasi za kiraia

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Mipango na Uwekezaji, Prof.Kitila Mkumbo, amesema serikali haitakuwa kikwazo kwa asasi za kiraia nchini, bali watatoa ushirikiano ili kuhakikisha wanapeleka maendeleo kwa wananchi.

Pia, amezitaka asasi za kiraia kutafuta na kutumia fursa ya rasilimali zilizoko nchini kuwasaidia wananchi kujikwamua kiuchumi na kuondokana na wimbi la umasikini.

Prof.Kitila, alisema hayo jana jijini Arusha, wakati akifungua wiki ya AZAKI kwa mwaka 2024, inayofanyika kwa siku tano na washiriki wako zaidi ya 600 mkoani humo.

Alisema kuna umuhimu kwa mashirika hayo yasiyokuwa ya kiserikali kushirikiana na serikali kutatua matatizo yanayowakibili wananchi kwa kuwa itasaidia kukuza uchumi wa nchi na kuwakwamua kiuchumi.

Hata hivyo, alisema serikali itahakikisha ustawi wa wananchi unakuwa na ili kufika lengo hilo na kila mmoja anapaswa kutoa maoni chanya katika uandaaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

Alisema endapo AZAKI kwa kushirikina na wananchi watatoa maoni italeta tija hasa katika suala la uwekezaji katika sekta za elimu, afya, maji, umeme, barabara, utalii, madini, ufugaji na kilimo.

"Hadi sasa asilimia 81 ya vijana kati ya miaka 15 mpaka 35, wameshatoa maoni mbalimbali kuhusiana Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Hivyo, tunatambua kwamba kuna changamoto kwenye suala la uchumi, lakini mnapaswa kufanya tathimini wapi nchi ilipotoka na tuendako,"alisema Prof.Kitila.

Aidha, alitaka kuzifundisha jamii namna ya kukabiliana na changamoto zinazowakabili ili kutafutwa kwa njia mbadala za utatuzi badala ya kuilalamikia serikali kwamba haifanyi kazi.

Naye Rais wa Foundation For Civil Society (FCS), Dk. Stigmata Tenga,alisema AZAKI hizo zina mchango mkubwa wa kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwa jamii kama zitafanya kazi zao kwa weledi.

Mkurugenzi wa TradeMark Africa, Elibariki Shammy, alipongeza mpango mkakati uliowekwa na serikali wa kuhakikisha biashara za kidigitali zinakua zaidi na kuhakikisha vijana wanakuwa sehemu ya mafanikio hayo.

Alisema wanashiriki kwa kasi kubwa katika biashara kwa kuweka mazingira wezeshi yatakayowasaidia wananchi wakiwamo vijana kujikaua kiuchumi kutokana na fursa zilizoko nchini.

# Mradi bomba la mafuta wafikia hatua muhimu

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MRADI wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) umefikia hatua muhimu katika eneo la Chongoleani, Tanga, ambapo Balozi wa Tanzania nchini Uganda, Jenerali Paul Simuli, ameelezea umuhimu wa mradi huu kwa uchumi wa nchi hizo mbili.

Jenerali Simuli, alisema bomba hilo ni fursa ya kipekee kwa uchumi wa Tanzania na Uganda na amefanya ukaguzi kuanzia unapoanzia mradi huo hadi Chongoleani ambapo ujenzi unaishia.

Kwa upande wa Uganda, alisema eneo la mradi na kwenye visima vya mafuta tayari wameshaweka sample zipatazo sita za kuvutia mafuta kutoka ardhini yalipo, lakini pia wametengeneza sehemu ya kuyahifadhia na kusafisha kidogo kuyaweka katika hali ya usafi.

"Ziara hii nchini nilianzia pale Kagera ambapo ndio tunayapokelea mafuta na shughuli nyingi za bomba hili zinaanzia pale, nizipongeze serikali zote mbili kwa kazi nzuri za kimaendeleo na kuitisha mikakati ambayo itazifanya nchi hizi kuwa na uchumi stahiki kwa wananchi wake," alisema.

"Vilevile kuwa na mahusiano mazuri ya kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi, lakini pia nimpongeze Rais wetu kwa kuweka nguvu yake yote katika mradi huu wa kimkakati unakamilika na kwa jinsi nilivyokuona unakwenda vizuri," alisisitiza.

Aidha, Balozi huyo alisema kulingana na maelezo na utekelezaji na jinsi alivyouona mradi huo matarajio ni makubwa kwamba utakelezaji utaendelea kuwa wa kiwango kinachokubalika lakini pia utamalizika kwa wakati.

Aliendelea kusema kuwa mradi huo wakati unaanza uliwajali wananchi na kuwapa fidia pesa taslimu na wengine walijengewa nyumba za kisasa, lakini pia ulitoa misaada mbalimbali kwa wananchi kulingana na jinsi mtu alivyoathirika kwenye eneo lake kuanzia ulipoanzia nchini Uganda.

"Kwa hiyo mradi umewagusa pazuri wale wote walioguswa, lakini umeweza kutoa elimu ya kilimo kwa wananchi wakulima katika maeneo yao kwa jinsi hani wanaweza kutumia eneo dogo kuzalisha, na wafugaji nao hawakuachwa nyuma.

"Walipewa elimu ya ufugaji bora na kujipatia kipato baada ya kuachia maeneo yao kupisha ujenzi huu wa kimkakati, hivyo basi niwaombe Watanzania, isiwe mradi huu tu, bali wowote ule ambao utakuwa wa kimkakati, tuwaige hawa wenzetu waliotoa maeneo yao kupisha maendeleo," alisema.

Alifafanua kwamba katika kambi zote alizopita wananchi wengi wamenufaika kwa kupata ajira ambazo ni za kudumu na za muda ambapo pia aliwataka kutumia fursa hizo kujiendeleza kwa kipato wanachopata kutokana na ajira zao.

"Labda tu niwaombe wale waliyopata zile ajira na kupata kipato, walinde ajira na kutumia vizuri kipato chao ili ajira zitakapofika mwisho, basi kipato kile kiweze kuwasaidia hata kupata mitaji na kuendesha maisha yao endapo watajioanga vizuri" alionya.





# Ushetu waanza mapambano dhidi homa ya ini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

IDARA ya Afya ya Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, imeanza kutekeleza agizo la Baraza la Madiwani la kuwataka kutoa elimu ya kujikinga na vimelea vya ugonjwa wa homa ya ini, baada ya kubainika kuwapo kwa baadhi ya watu wenye dalili za ugonjwa huo.

Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Athumani Matindo, aliyasema haya juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake vilivyotaka kujua ni hatua zinazochukuliwa baada ya agizo hilo lililolenga kuwanusuru wananchi dhidi ya tatizo hilo.

Dk.Matindo alisema wataalamu wa afya tayari wameanza kuzitembelea baadhi ya familia zilizodaiwa kuwa na wagonjwa wa homa ya ini na kuwafanyia vipimo ikiwemo kuwapatia elimu ya kujikinga dhidi ya ugonjwa huo.

Alisemwa wataalamu hao wamekuwa wakitoa elimu ya dalili za ugonjwa huo zinavyokuwa ili watakapombaini mgonjwa watoe taarifa kituo cha afya haraka.

Matindo alisema, katika kikao cha baraza la madiwani cha Agosti 28 mwaka huu kulitolewa hoja na baadhi ya kuwepo kwa watu wanaodaiwa kuugua ugonjwa wa homa ya ini katika moja ya familia katika Kata ya Bulungwa na kuagiza wataalamu wa afya waliofika na kushughulikia tatizo hilo.

Aidha alisema, agizo hilo wameshaanza kulitekeleza katika vituo vyote vya afya vya halmashauri hiyo kwa watalaamu kuwapima wananchi na kutoa elimu ya njia ya kujikinga na maambukizi ya vimelea vya ugonjwa huo.

Alisema kwa wajawazito wanaofika kufahamu maendeleo ya afya zao nao wanapewa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi, akiwemo mkazi wa Ubagwe, Matrida William aliomba washirikishwe watoa huduma ngazi ya jamii ambao muda wote wapo karibu na wananchi.

Alisema wataalamu hao wanauwezo wa kuongea lugha ya asili ili kuhakikisha elimu hiyo inawafikia wananchi wengi.

# Chanzo matukio ya moto Sengerema chatajwa

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WANANCHI wilayani Sengerema mkoani Mwanza wametahadharishwa tabia za kuwaachia watoto vitu vinavyohusiana na moto, ambavyo vimekuwa vikisababisha matukio hatarishi hivi karibuni wilayani hapa.

Tahadhari hiyo imetolewa jana na Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wilaya hapa, Juma Ngwembe wakati akizungumza na Nipashe juu ya vyanzo vya matukio ya moto ambayo yamekuwa yakitokea na kufanyiwa uchunguzi na jeshi hilo.

Ngwembe alisema sehemu kubwa ya matukio hayo yamekuwa yakisababishwa na wazazi kuwaachia watoto vifaa vya moto ambavyo huvitumia tofauti na kusababisha kuwaka moto wakati mwingine kusababisha vifo kwa watoto hao.

Aidha, alisema ili kudhibiti matuki hayo ni vyema wazazi kuwa makini na vitu hivyo vikiwemo viberiti, vibatari pamoja na mishumaa.

**Alisema kumekuwa na desturi ya baadhi ya wazazi kuwaachia watoto shughuli za kupika kitu ambacho ni hatari hasa kwa wale ambao hawatambui njia za kujikinga na shoti**

Alisema kumekuwa na desturi ya baadhi ya wazazi kuwaachia watoto shughuli za kupika kitu ambacho ni hatari hasa kwa wale ambao hawatambui njia za kujikinga na shoti za umeme pamoja na moto.

Alisema: "Mfano mtoto anaweza kugusa maji na kwenda kushika nyaya zilizoungwa hali inayoweza kusababisha mlipuko wa umeme au yeye mwenyewe kupoteza maisha kabisa, hivyo wazazi wa namna hiyo waache kabisa na wajitahidi kuwa makini na watoto wao".

Mkazi wa wilayani hapa, Emmanuel John alisema matukio ya moto yanarudisha nyuma maendeleo katika jamii, hivyo kuahidi kuendelea kuchukua tahadhari juu matukio hayo na kuliomba jeshi hilo kujitahidi kuwahi pale linapohitajika.



Mwandikishaji wa daftari la kudumu la mpigakura (kulia), akiandika maelezo ya mmoja wa wakazi wa mjini Musoma, wakati wa siku ya mwisho ya kuboresha daftari hilo, mkoani Mara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aweso atoa maagizo RUWASA kuhusu mfumo wa malipo

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameuagiza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kuweka mfumo rahisi wa malipo ya Jumuiya za Watumiaji Maji (GEPS) ili kupunguza malalamiko kwa wateja wao.

Aweso alitoa agizo hilo jana wakati akiweka jiwe la msingi katika mradi wa maji katika Kata ya Bwanga wilayani Chato mkoani Geita, wenye tangi lenye ujazo wa zaidi ya lita 200,000 ambalo ujenzi wake umegharimu Sh.bilioni 1.6.

Pia alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Mwajuma Waziri, kushirikiana na RUWASA ili kuwezesha mfumo huo kuingiza na kutoa fedha za bili ya maji haraka kwa ajili ya kuwarahisishia wananchi malipo.

Awali Mbunge wa Jimbo la Chato, Medardi Kaleman, alisema jumla ya miradi 16 ya maji imetekelezwa jimboni humo na kusaidia kuongeza hali ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Aidha baadhi ya wananchi wa Kata ya Bwanga waliishukuru serikali kwa kusogeza mradi huo wa maji, wakisema utaondoa adha ya ukosefu wa maji wanayokabiliana nayo kwa muda mrefu sasa.

# Mkunga asimulia madhira wajawazito waliokeketwa

**Na Timothy Itembe,** TARIME

MKUNGA kutoka Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Esther Ghati, amesema wajawazito waliokeketwa wanapitia changamoto kubwa wakati wa kujifungua, ikiwamo kutoka damu nyingi na kuisisitiza jamii kushirikiana kupinga vitendo hivyo. Ghati akibainisha hayo juzi, kwenye mdahalo wa mradi wa 'jamii imara' unaotekelezwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika Tanzania chini ya ufadhili wa ubalozi wa Marekani.

Alisema wanawake ambao wamekeketwa wakati wa kujifungua njia yao inakuwa ndogo hadi watafutiwe njia mbadala ya kupanua wakati wa kujifungua hali inayowasababishia maumivu makali pamoja na kumwaga damu nyingi.

Kufuatia hali hiyo aliitaka jamii kuungana pamoja kukemea ukeketaji akitaja vitendo, hivyo kutokuwa na tija ili kupunguza na kudhibiti kabisa vifo vya mama na mtoto.

Aidha Ghati alionesha kutokukubaliana na wale wote ambao wanaosema kuwa ukeketaji unachochewa na wazee wa mila na kutoa ushuhuda wa mzee wa mila kijijini kwao mwenye watoto wakike ambaye hajawakeketa licha ya kuwa mke wake anapenda watoto wakeketwe.

Alisema mzee hiyo anafanya njama ya kuwatorosha mabinti zake kwenda kuwaficha katika mkoa mwingine kama Dar es Salam ili wasifanyiwe kitendo hicho. Ofisa Mradi wa Jamii Imara, Suzan Kawanga alisema kama wadau hawawezi kutokomeza mila za watu bali jukumu lao ni kuhakikisha wanatoa elimu ya madhara yatokanayo na mila potofu ikiwemo ukeketaji, ili jamii ielimike na kuachana na vitendo hivyo.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 12, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## Bingwa afya akili, awaonyesha vijana njia sahihi kukwepa madhara ngono



## JANABI, TIBA PUTO NA MAMBO YAKE... Vicent alivyotimiza lengo kutoka kilo 150 hadi 90; kiuno chake inchi 50 hadi 36..

Ukurasa 12

### VIFO UZAZI VYAPUNGUA 80%

# Samia akiinakishi afya kupitia MMAM ya JK; Mama & Mtoto, Afya ya Msingi

**Na Peter Orwa**

KITAALUMA, afya maana yake ni hali ya ukamilifu kimwili, kiakili, kijamii na kutokuwapo maradhi kwa mtu.

Hivi sasa kuna juhudi zinazochukuliwa kimataifa kukabili afya kwa namna mbalimbali, ikiwamo jozi inayojulikana kama 'afya ya mama na mtoto.'

'Afya ya Mama na Mtoto' imo katika yaliyounganishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ulioasisiwa mwaka 2007 na kuanza kufanya kazi 2008, serikali ikiendeleza chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Kuzaliwa kwa MMAM chini ya Rais Jakaya Kikwete, kuliendana na kubuniwa Sera ya Afya, iliyochukua nafasi nyingine ya mwaka 2000.



Dorothy Gwajima, alipokuwa Waziri wa Afya, akiwa amembeba mtoto katika Siku ya Chanjo kwa Watoto Kitaifa. **PICHA: MTANDAO.**

Katika tafsiri yake inaipatia nafasi "Afya ya Mama na Mtoto', kwa kutoa mwongozo maalum kwa wanawake walio na umri wa uzazi na watoto umri chini ya miaka mitano, hasa siku 28 baada ya kuzaliwa.

Pia, kuna Afya ya Msingi. Historia yake, ina mzizi unaoanzia baada ya mkutano wa kimataifa ulioandaliwa mwaka 1978 na Shirika la Afya Duniani (WHO) na shirika lingine la Umoja wa Mataifa - Linaloshugulikia Watoto (UNICEF).

Hilo lilikubaliwa na nchi wanachama wa WHO kama hatua muhimu kufikia lengo la 'afya kwa wote', kwa vile kulikuwapo vifo vingi duniani na watu hawakuwajibika sana na mifumo ya afya.

Kwa mujibu wa WHO, 'Huduma ya Afya ya Kimsingi' unatajwa "Utaratibu unaoangazia afya na uzima wa jamii, huduma hizo zikijikita kwenye mahitaji na matakwa ya watu binafsi, familia na jamii.'

Hilo linatajwa na shirika hilo, kwamba "linagusa huduma zote za afya kwa mtu katika maisha yake yote, sio tu kwa maradhi fulani' na kuna vipengele muhimu vilijumuishwa;

Kuhakikisha usambazaji dawa za kutosha, kuondoa vikwazo vya fedha na kupatikana ulinzi wa afya ya kijamii.

**AWAMU VI NA VIFO**

Ndani ya muda si mrefu baada ya Rais Dk. Samia kuingia katika uongozi, aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa ufafanuzi wa msisitizo wa afya ya mama na mtoto, kwa viongozi wa mikoa na halmashauri, kuwapa ushirikiano timu ya madaktari bingwa wa Rais Dk. Samia waliopelekwa mikoani kuhudumia wananchi.

"Tumsaidie Rais Samia kuvunja rekodi nyingine duniani ya kupunguza vifo vya watoto wachanga, kwa kuwa vifo hivyo tumevipunguza kwa asilimia nne tu, kutoka vifo 25 katika kila vizazi hadi 1,000 hadi vifo 24 katika kila vizazi hai 1,000, takwimu za mwaka 2020/22," alitamka Ummy.

Katika mfano mmojawapo wa operesheni hiyo wakati huo, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Mama na Mtoto (wakati huo) Dk. Felix Bundala, akasema katika siku tano, mikoa ya Tanga, Ruvuma, ni kwamba:

"Kati ya wateja 6,381 walioonwa, waliofanyiwa upasuaji ni 166 sawa na asilimia tatu, waliopewa rufani ni 42 ambao ni sawa na mtu mmoja kati ya watu 100, amepata rufani."

Ni baada ya miaka miwili, Rais Dk. Samia, akawa na matunda yenye rekodi duniani, kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 80, ikiwa ni takwimu kutoka vifo 556 kati ya vizazi hai 100,000 hadi vifo 104; awali ilitokea asilimia nne.

Ni hali inayogusa tamko na azimio lake la awali kwamba: "Tumsaidie Rais Samia kuvunja rekodi nyingine duniani ya kupunguza vifo vya watoto wachanga...."

**MPANGO UNAVYOENDELEZWA**

Katika mwndelezo wa 'Mpango Kabambe wa Madaktari Bingwa wa Rais Dk. Samia', unalenga kupunguza vifo vya watoto wachanga na kuwajengea uwezo watoa huduma katika hospitali za halmashauri.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, katika taarifa yake ya Mei mwaka huu, panalengwa kuwapo Wodi Maalum za Watoto Wachanga (NCU) katika hospitali hizo za mikoa, ili kuokoa maisha ya watoto wachanga na hasa wenye umri chini ya siku 28.

Huduma hiyo aliyoizindua Waziri, ililenga huduma za kibingwa kwenye hospitali 184, katika ngazi ya halmashauri, waendeshaji wake wakiwa Madaktari Bingwa wa Dk. Samia, wenye kaulimbiu "Tumekufikia, Karibu Tukuhudumie".

"Nasisitiza tena kwamba, sambamba na utoaji huduma na kujenga uwezo wa watoa huduma wetu, madaktari bingwa saidieni uanzishaji na kuimarisha utendaji wa NCU kwa kuwa katika mpango huu, mtafikia hospitali zote za halmashauri (nchini)." akasisitiza Waziri.

Waziri Ummy akamtaka kila mwanamke mjamzito anayefika hospitali kwa ajili ya kujifungua, anatakiwa atoke salama yeye na kichanga chake.

"Tunaweza kuokoa maisha ya watoto wachanga endapo tutaanzisha wodi maalum za watoto wachanga, tukaviwekea vifaa tiba ili endapo mtoto akiwa na changamoto yoyote aweze kupata huduma," anasisitiza Ummy.

**HUDUMA DHARURA**

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Charles Mahera, anamsifu Rais Dk. Samia, kwamba hadi Januari mwaka huu,

Inaendelea Uk. 14

AFYA

## JANABI, TIBA PUTO NA MAMBO YAKE...

# Vicent alivyotimiza lengo kutoka kilo 150 hadi 90; kiuno chake inchi 50 hadi 36...

- Watoto: Mama, baba anaumwa nini?; mitaani 'ni yeye au ndugu yake?'
- Aliendesha gari asubuhi akawekewe, jioni akarudi analo tumboni
- Asimulia alivyokuwa mpenda kula, baada ya kuwekewa, wa kawaida

**Na Christina Mwakangale**

MWONEKANO mpya wa mwili wa Vicent Fortunatus, una tafsiri tofauti. Kwanza amefanikiwa kuyakabili magonjwa yasiyoambukiza (NCDs).

Jamii, familia nayo inatafsiri yake kwa mwonekano mpya wa Vicent. Wapo wanaomshangaa, baadhi wakimwangalia kwa ishara ya kiulizo, wakiogopa kuuliza kwa nini kapoteza uzito kwa kiwango kikubwa.

Walio na ujasiri wanamuuliza kila wanapokutana naye kwamba ni yeye halisi au nduguye. Familia nayo inashangaa. Mtoto wake aliyerejea nyumbani kutoka shule ya bweni na kumkuta baba yake amepungua, alimnong'oneza mama: "baba anaumwa nini..."

Prof. Janabi, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), katika kitabu chake 'Mtindo wa Maisha na Afya Yako', anamwelezea Vicent, akimtaja ni miongoni mwa mashuhuda wa simulizi halisi katika kubadili mtindo wa maisha, kuepuka NCDs.

Prof. Janabi, mbali na kuwa mtendaji mkuu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), pia mwanataaluma, tabibu bingwa kwenye magonjwa ya kundi la NCDs na Mkaguzi wa Matibabu Usafiri wa Anga aliyeidhinishwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Marekani (FAA-USA), anasema:

"Vicent, amefanyiwa tiba maalumu ya kuwekewa puto katika tumbo na matokeo yake amekuwa mwepesi na kuumudu mwili wake sawasawa.

"Kwa mfano, anaeleza (Vicent) kwamba alikuwa amefikia hatua ya kushindwa hata kukunja mguu, sasa anaweza kukunja mguu kwa saa kadhaa bila maumivu yoyote."

Anaeleza kupunguza uzito kutoka kilo 150 hadi 99, amepunguza ukubwa wa kiuno chake kutoka inchi 50 hadi 36. Daktari anamtaja ameepuka kupata kisukari; magonjwa ya moyo na shida ya kiharusi.

Vicent, mkazi wa Mabibo-External, Dar es Salaam, amewekewa puto kwenye utumbo wake mwezi Januari mwaka jana, kupunguza kilo 150 alizokuwa nazo kipindi hicho, sasa ameanza safari ya maisha mapya, baada ya safari ya siku takribani 385; ni mwaka mmoja na siku 20 za kukabiliana na tauzo la uzito.



Vicent Fortunatus wa zamani. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE.**

### MWANZO WA TIBA

Prof. Janabi anaeleza kuwa, puto huwekwa tumboni kuchukua nafasi ambayo ni sawa na theluthi moja ya ukubwa wa tumbo.

Katika utaratibu huo wa kuweka puto tumboni, mgonjwa hapewi 'nusu kaputi', isipokuwa dawa kidogo ya usingizi inayomfanya mwili uwe katika hali ya kupumzika (relaxed), kufanikisha shughuli hiyo.

Kwa kawaida, ndani ya puto, huwekwa maji ya chumvi chumvi kiasi cha nusu saa, ili kulifanya litulie sehemu moja na hukaa tumboni kwa kipindi cha miezi sita hadi nane.

Hata hivyo, kuna wengine wanaokaa nalo kwa kipindi cha miezi 12, wakijifunza kula chakula sahihi kwa wakati sahihi.

Baada ya kuondolewa puto, mgonjwa anaendelea na mtindo mpya wa maisha, kula kwa usahihi, akiulinda mwili wake usirejee uzito wa awali.

Mnamo Januari 2023, MNH-Mloganzila iliwawekea puto takribani wagonjwa 180, akiwamo Vicent pamoja na wengine ambao walifanyiwa upasuaji wa kupunguza ukubwa wa tumbo (Gastric sleeve).

Prof. Janabi anasema, Vicent amefanikiwa kupunguza uzito wa mwili wake, baada ya kuwekewa puto na alipozungumza naye, akaeleza faraha ya nafuu aliyopata kutokana na tiba hiyo, kupunguza kilo 51.

Anaeleza alipata taarifa za kuwako huduma hiyo kupitia redioni, naye akachukua hatua kuwatafuta wahusika. Aidha, aliwasiliana na hospitali akapewa kupewa miadi kuonana na madaktari wanaofanya shughuli hiyo.

Prof. Janabi anaeleza, kwamba Vicent anakiri kabla ya kwenda Mloganzila alifanya utafiti wake binafsi kupitia mtandao wa intaneti.

Taarifa alizopata zilimthibitishia kwamba, njia ya kuwekewa puto ni bora kumsaidia kupunguza uzito na akafurahi kuona hilo linapatikana nchini.

Anasimulia kwamba, ingawa alikuwa anafanya mazoezi ya kupunguza uzito, matokeo yake hayakumtia moyo sana, kwani mwili ulipungua taratibu na wakati mwingine akapumzika kufanya mazoezi kwa siku chache, labda kwa sababu ya uchovu, mwili ukaongezeka zaidi.

Vilevile, Vicent anaeleza namna alivyoendesha gari lake hadi hospitalini Mloganzila, mnamo Januari 10, 2023 na siku hiyo hiyo akawekewa puto na jioni ya saa 10, aliruhusiwa kuondoka hospitalini hapo akiendesha tena gari lake kurejea nyumbani.

### HATUA ZA MATIBABU

Mgonjwa ni lazima awe na walau kilo 90 na kuendelea. Anakuwa na uchaguzi wa nini cha kufanyiwa. Katika kundi la waliofanyiwa matibabu hayo, aliyekuwa na uzito wa chini kabisa ni mwenye kilo 110 na wa juu kilo 124.



Vicent Fortunatus, baada ya kuwekewa puto.

Prof. Janabi anaendelea kumwelezea Vicent, alitakiwa ale chakula mwisho saa mbili usiku kuamkia siku ya kuwekewa puto.

Alipewa dawa ya usingizi ya kuanzia dakika 15 hadi 20. Puto liliingizwa tumboni kupitia njia ya mdomoni.

### MADHARA ALIYOPATA

Vicent anasimulia, alihisi kichefuchefu kwa muda wa siku nne za mwanzo, kwa sababu ni mfumo wa mwili kujilinda kutokana na kuingia kitu kipya na kilichomo tumboni kutaka kukitoa. Hali hiyo, Prof. Janabi anaifafanua inafanana na wanayopata wajawazito miezi mitatu ya awali.

Hata hivyo, taarifa kutoka hospitali zinasema waliowekewa puto tumboni, kati ya hao wawili tu ndio walishindwa kuendelea kukaa nalo hadi mwisho.

Hao walipatwa na hali ya kichefuchefu na kutapika kusikovumilika, matokeo yake waliondolewa maputo hayo.

Waliobaki 180 kama ilivyo kwa Vicent, waliendelea na mchakato wa kupunguza uzito wa mwili, Prof. Janabi: "Kwa mfano, Vicent katika siku 10 za mwanzo aliona mabadiliko makubwa, hakuwa anahisi sana njaa na alihisi kutosheka kabisa.

"Mwili ulipoteza uzito mkubwa kwa usalama; uzito unashuka taratibu. Ngozi ya mwili haitepeti kutokana na mwili kupungua.

### VICENT MPYA

Prof. Janabi anaeleza, Vicent amekuwa mwepesi na kuumudu mwili wake sawasawa, akitoa mfano, anaeleza alikuwa anafikia hatua ya kushindwa hata kukunja mguu, lakini sasa anaweza kukunja mguu kwa saa kadhaa bila ya maumivu yoyote.

Lingine, ambalo ni kuu ni kwamba Vicent wa sasa amepunguza uzito kutoka kilo 150 hadi 99, ukubwa wa kiuno chake kutoka inchi 50 hadi 36, pia maumivu ya mgongo yametoweka.

Anakumbuka namna Vincent, kila alipoikaa kwa saa nne tu, alikuwa akipata maumivu makali ya mgongo, nayo yameondoka.

Vicent anasimulia kwamba, alikuwa hawezi kuchuchumaa na ikawa vigumu kwake kutumia vyoo vya namna hiyo.

Hali yake ya sasa, pia ameacha utumiaji dawa za kupunguza maumivu, kwa kuwa maumivu ya viungo na mgongo hayapo tena na ufanisi wake katika kufanya kazi umeongezeka, huku akiacha utaratibu wa kula au kufungasha vyakula kila mara.

Anasema, alitumia dawa za kuondoa maumivu, ambazo haziondoi tatizo la maumivu mwilini, bali zinaahirisha kwa muda, kwani tatizo linaloleta maumivu lilikuwa halijatibiwa.

Dawa hizo pia zina uwezekano mkubwa wa kuleta matatizo mengine ya viungo vya mwili, kama figo na kuibuka kwa vidonda tumboni.

Anasema, utatuzi wa maumivu ya magoti na mgongo ni kufanya mazoezi na kupunguza uzito.

### JAMII NA VICENT MPYA

Vicent, shuhuda wa watu waliowekewa puto ana simulizi yake, kwamba watu wanamshangaa sana wakiona amepunguza uzito wake na baadhi ya watu wakimwangalia kwa anayoita 'macho ya maswali' mengi, lakini wanaogopa kumuuliza kilichompata, hata kupoteza uzito kwa kiwango cha juu namna hiyo.

Anaeleza kuwa wengine wanaokutana naye, wamekuwa wakihisi huenda ni ndugu yake wa karibu, lakini mshangao huo huenda unafika mbali kwenye familia.

Vicent anatoa mfano wa mtoto wake aliyerejea nyumbani kutoka shule na kumkuta amepungua, alimshangaa na kuduwaa akiamini kwamba baba yake anaumwa.

Akamuuliza mama yake kwamba, baba anaumwa nini, baada ya kuona alivyopungua na Vicent anaeleza kumekuwapo woga ndani ya familia, hata mkewe anaangukia hoja, akimwambia 'anawatisha watoto kwa kupungua sana' na kumshauri akalitoe puto.

> "Mwili ulipoteza uzito mkubwa kwa usalama; uzito unashuka taratibu. Ngozi ya mwili haitepeti kutokana na mwili kupungua.

### ANACHOEPUKA VICENT

Prof. Janabi anasema, faida ya mabadiliko hayo ya uzito ameepuka maradhi yasiyoambukizwa, kaepuka kupungua nguvu za kiume: kukoroma wakati wa kulala; na kuepuka kukata pumzi.

Tabibu huyo bingwa, anashuri jamii ijue wazi kwamba, njia hiyo ya kujiepusha na magonjwa hayo ni rahisi na isiyokuwa na gharama.

Faida kubwa zaidi anayoitaja, ni magonjwa anapata faida na nafuu kubwa ya maisha. Kwa hiyo watu wanashauriwa kubadili mtindo wa maisha kuhusu ulaji, kuchagua unakula chakula gani, kutambua unakula saa ngapi.

Pia anashauri watu kufanya mazoezi, walau kutembea hatua 10,000 kwa siku, kuepuka pombe na kuacha kuvuta sigara.

Anataja madhara ya uzito uliopitiliza ni makubwa kwa ustawi wa jamii. Kama ilivyo kwa mataifa yaliyoendelea, bara la Afrika nalo limekumbwa na athari za wagonjwa wenye uzito uliopitiliza.

Wakati wa mlipuko wa maradhi ya Uviko-19 kwa miaka mitatu iliyokuwapo, iliua takribani watu milioni sita duniani kote, lakini magonjwa yasiyoambukiza yanaua watu wengi, zaidi ya mara nne ya vifo hivyo kwa mwaka.

Prof. Janabi anataja magonjwa yanayowapata watu kutokana na kuchochewa na uzito uliopitiliza ni kisukari; magonjwa ya moyo; shinikizo la juu la damu; kiharusi; magonjwa ya figo; kukosa hamu ya tendo la ndoa; ugumba na msongo wa mawazo.

### MASHARTI YA PUTO

Prof. Janabi anasema anayetakiwa kupatiwa tiba hiyo ni ambaye hana vidonda vya tumbo; hana ngiri ya chembe ya moyo; hana matatizo ya damu; hana ugonjwa wa ini: hatumii dawa za kulevya; na hajawahi kufanyiwa upasuaji wowote wa tumbo.

Madhara ya siku chache ni kama vile mgonjwa, ni kwa haja kubwa kufunga kwa muda (Kuvimbiwa); Asidi kujaa tumboni; mkwaruzo wa koo: puto kupasuka na maji yakatoka, na humtokea kwa wastani wa mgonjwa mmoja kati ya 1,000; pia, maumivu ya muda mfupi ya kongosho; na michubuko midogo.

Prof. Janabi ana wito wa vyakula vinavyotakiwa kuepuka uzito ni vya ngano isiyosindikwa; jamii ya kunde isiyosindikwa; jamii ya ulezi; choroko; mchele wa kahawia (brown rice);

"Kundi hili la chakula linatajwa kutokuwa na kiwango kikubwa cha sukari. Pia kula mboga za majani, matunda kama ilivyo, kuliko kukamua juisi.

Pia, anataja vyakula vya protini kama nyama; kuku: mayai; samaki; mafuta yanayotokana na mimea kama ya nafaka, alizeti, karanga, mawese, pamba, mafuta ya mizeituni, yanafaa."

AFYA

# Bingwa afya akili, awaonesha vijana njia sahihi kukwepa madhara ngono

Na Joyce Lameck



Vijana katika mjumuiko wao. Ni mahali sahihi pa kupatiwa elimu ya afya yao na ngono. **PICHA: MTANDAO**

KATIKA jamii nyingi, bado kuna imani ya kumpa elimu kijana kuhusu afya ya uzazi, kunachochea vishawishi vya kuanza ngono katika umri mdogo na kuwaletea madhara katika ukuaji wao.

Lakini, mzazi anatakiwa kukumbuka, pasipo elimu kwa kijana wake anaweza kupata elimu ya watu tofauti na kuangukia matokeo hasi kwa siku za baadaye.

Mbali na jamii inayomzunguka, kuna utandawazi ulioteka akili za vijana wengi sasa na huenda anaweza kujifunza vitu kupitia mitandao ya kijamii katika kupata darasa lolote analohitaji kujifunza.

Stahiki ya vijana ni kupatiwa elimu sahihi ya afya ya uzazi kupitia mtandao, kuna sababu teknolojia inayokua kwa kasi duniani na vijana wengi wanaitumia kutoa au kupokea taarifa mbalimbali.

Baadhi ya mitandao imekuwa ikitoa elimu isiyo sahihi kwa vijana na wanaamua kwa njia isiyo sahihi, kuhusu mambo ya uzazi salama na hata kuleta madhara kwa kundi kubwa la vijana.

Ili wapate taarifa sahihi za afya ya uzazi, wanapaswa kufuatilia idhaa za radio au televisheni zinazotoa zaidi elimu na sio habari zile za udaku, kwa sababu mara nyingi vinaandaliwa vipindi maalumu vya kuelimisha.

### BINGWA AELEZ A

Mratibu wa Kitaifa wa Masuala ya Afya ya Uzazi wa Vijana na Jinsia, Dk. Gerald Kihwele, alisema kuwa vijana wanapaswa kupata taarifa sahihi kutoka kwenye idhaa sahihi kwani hiyo ni changamoto kubwa inayowakumba vijana.

Msomi huyo wa afya ya akili, mwenye umri ulioko 'mitaa ya ujana' na uzoefu wa kutumika katika Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe, jijini Dodoma, ana ushauri kwa watoa huduma za afya, watumie idhaa zinazopendwa na vijana za redioni, kuwafikisha elimu hiyo kirahisi.

Anaitaja kuwa staili bora, maana somo hilo hilo redioni au kwenye televisheni kuhusu afya ya uzazi, mara nyingi zinakuwa na watu maarufu, wenye weledi na wepesi kufanikisha uelewa wao.

Dk. Kihwele anasema, wazazi wanapaswa kutafuta namna ya kuzungumza na vijana wao, jinsi ya kutumia mitandao hata kuweza kupata elimu kuhusu afya ya uzazi na si kuweka mazingira ya kuwafanya vijana kuona suala hilo ni kosa.

Kipindi cha umri wa ama balehe au 'binti kuvuka awamu ya kwanza' ni mabadiliko ya kimwili, kitabia na kihisia, hata wanapofanya uamuzi wanakuwa na taarifa za kutosha kuhusu afya yao ya kingono, sambamba na mabadiliko hayo ya afya ya uzazi.

Eneo lingine analolitaja mtaalamu huyo, ni haja ya kijana anapoangukia stahiki ya kufikiwa na maarifa, vilevile ujuzi unaohusiana na huduma za afya, anakuwa katika nafasi bora na wenye taarifa sahihi za afya, pia uzazi salama unaogusa maisha ya ngono.

Ni taarifa zinazowasaidia vijana kuchelewa kuanza vitendo vya ngono, wakihitaji pia 'kingamimba' wakati wanapoamua kufanya ngono. Vyote vinajielekeza katika namna ya kuwa na taarifa zinazomfaa kiumri, kuhusu ngono salama na afya bora ya uzazi na ukuaji wake.

Ngome ya taarifa tajwa inagusa uhusiano, maadili, mtazamo, stadi, utamaduni, jamii na haki za binadamu katika ukuaji, zikigusa mwenendo wa kingono na afya ya uzazi, vijana kupata uelewa unaowahusu.

Kisaikolojia na kijamii, watoa huduma wanahitaji kuhakikisha vijana wanapata maarifa na huduma wanazozihitaji, ili kujilinda na wengine dhidi ya madhara yasiyokusudiwa kingono, ikiwamo maambukizo ya magonjwa ya zinaa na mimba zisizotarajiwa.

Wataalamu wanataja nafasi nyingine wanayopswa kupewa vijana, ni ushauri kuhusu maisha ya balehe, viungo vya uzazi, ngono, mzunguko na mwenendo wa wa maisha ya kingono na mwitiko wake, vyote vitawasaidia kuwa makini kufanya uamuzi sahihi.

### UZUIAJI MIMBA

Katika jukumu la kuzuia mimba, suala la kutoa kingamimba za dharura, pia kuelewa, kutambua na kupunguza uwezekano wa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ni muhimu.

Ukuaji teknolojia duniani, inawafanya watu wengi sasa wanatumia mitandao katika utoaji elimu tofauti, zinazosaidia jamii kupata uwelewa wa kutosha unaohusu masuala mbalimbali.

Hata hivyo watoa huduma za afya ni vema wakatumia mitandao katika kutoa elimu na mafunzo kuhusiana na afya ya uzazi, kwani kwa sasa si rahisi kijana kwenda hospitali kwa ajili ya kupata elimu juu ya uzazi.

vijana wakiwa katika hatua, bado hawajaitwa baba au mama, inawafanya wengi kushindwa kupata elimu sahihi ya uzazi na kuwawezesa kufikia uzazi salama.

Elimu ya Afya ya Uzazi kwa vijana inawapatia maarifa ya kujitambua, kufahamu mabadiliko yanayoweza kuwatokea pindi wanapoendelea kukua na namna ya kufanya maamuzi sahihi ya kuwa hali ya kukosa elimu sahihi ya uzazi imekuwa ikileta madhara.

Kuna vijana sasa wanapata mimba, wakati hawana elimu sahihi ya uzazi, ilhali wana na 'simu janja'. Hivyo, kuwapo makundi sahihi ya vijana mitandaoni, yanasaidia vijana wengi kupata taarifa sahihi juu ya afya ya uzazi na kutokomeza dhana za kizamani kuhusu uzazi.

Vile vile kuwapo na majukwaa ya kidijitali katika mitandao, yanayozungumzia afya ya uzazi salama kwa vijana na kuwapa fursa ya kuuliza maswali na ufafanuzi sahihi, nayo yana umuhimu wake.

Mustakabali mpana wa elimu ya uzazi kwa vijana, inmavuta majibu na haki kwao kuyajua, hivyo washirikio kuyadhibiti magonjwa mengi ya zinaa nchini, kama vile kaswende na Ukimwi.

## SAMIA AKIINAKISHI AFYA KUPITIA MMAM YA JK; MAMA & MTOTO, TIBA YA MSINGI

Inatoka Uk. 11

alishawekeza katika huduma za dharura (EMD) nchini, sehemu 80 kuna huduma za Wagonjwa Mahututi (ICU), 28 ni afya ya msingi, zimekamilika na zinatoa huduma.

Kwa nafasi ya pekee, akataja jengo la wagonjwa wa dharura katika Hospitali ya Wilaya Makete, ambako alizungumza kwamba iko katika orodha hiyo, chini ya 'uwekezaji wa Dk. Samia.'

Mwanzo wa mwaka huu Dk. Mahera amemsifu rais, kwamba anaendelea kuboresha sekta ya afya, akitumia mfano wa kununuliwa magari 316 ya kubeba wagonjwa kwa matarajio ya kusambazwa ngazi ya afya ya msingi, kuwahudumia wananchi penye hitaji la rufani.

Ni aina ya uwekezaji uliofanyika kwa mwezi huo Januari mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Albert Chalamila, anapomtaja Rais Dk. Samia, anaendeleza katika sekta ya afya; hususani 'huduma ya mama na mtoto', kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pingamizi.

Ni tamko lake Chalamila, alipokuwa akiwakabidhi wabunge wa majimbo 10 ya mkoa wa Dar es Salaam, vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 691, vilivyotolewa na serikali.

Akasema, vifaa hivyo ni miongoni mwa vilivyozinduliwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu mwezi huo, kwa nchi nzima vikiwa na thamani ya shilingi bilioni 14.9 kwa majimbo na halmashauri 214 nchi nzima.

Chalamila akiwa mwakilishi wa Rais kimkoa, huku tukio hilo akifanya kwa niaba ya Waziri Ummy, anasema mkuu wa nchi amedhamiria kumaliza vifo vinavyosababishwa na uzazi, hivyo uwekezaji mkubwa unaendelea kufanyika katika sekta hiyo.

Kwa mujibu wa Chalamila, mkoa wake umepewa zaidi ya shilingi bilioni 52, kuimarisha sekta ya afya na wanaboresha kujenga vituo vipya vya afya na kuiwezesha Mamlaka ya Dawa (MSD) kusambaza vifaa tiba vya kisasa katika vituo vya umma.

### HATUA ZA DUNIANI

Hadi sasa dunia inatajwa kumepiga hatua kubwa katika kupunguza vifo vya kinamama, wajawazito na Watoto, hasa wachanga walioko katika mazingira dhaifu kiafya na mama zao, wanaokabiliwa na vikwazo vya kupata huduma bora za kuwaokoa kimaisha.

Mamlaka za afya na jamii duniani, zinafafanua kwamba kifo cha mwanamke wakati wa ujauzito au kujifungua, kinatishia uwezekano wa mtoto wake kuishi na kinapunguza nafasi za watoto wake wengine kuishi na elimu, hata kutishia utulivu wa familia yake.

Hatima yake, inatajwa kwamba vifo vya kinamama na watoto wachanga, vinadhoofisha ustawi wa nchi. Takwimu za msimu wa miongo miwili iliyopita, ni kwamba vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kwa wastani asilimia 40 tangu mwaka 2000, pia vifo vya watoto wachanga vimepungua wastani asilimia 50 duniani, tangu mwaka 1990.



## HABARI DODOMA

# Kampeni kupima UKIMWI kuanza Dodoma

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

OFISI ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Idara ya Afya imeanzisha huduma za upimaji virusi vya Ukimwi kwa makundi yaliyoachwa nyuma wakiwamo vijana na wanaume ili kuongeza kasi ya kudhibiti maambukizi.

Kupitia huduma hiyo chini ya mradi wa USAID Afya Yangu Kanda ya Kaskazini wataalamu wa afya wataweka kambi kwenye viwanja vya michezo jijini hapo yanapofanyika mashindano ya mpira wa miguu maarufu kama 'Ndondo Cup' na kuwahudumia wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini humo, Meneja Mradi Mwandamizi wa USAID Afya Yangu Mkoa wa Dodoma, Dk. John Kashindye, alisema huduma hiyo utekelezaji wa mapambano dhidi ya maambukizi ugonjwa huo kwa kuwafikia asilimia 95.

"Asilimia 95 ya kwanza ya malengo ni kwamba wale watu wote wanaoishi na maambukizi ya virusi vya Ukimwi asilimia 95 tuwe tumewafikia ifikapo 2030 na 95 ya pili ni hao ambao watakuwa wameshajua hali zao waweze kupata matibabu ya kufubaza."

Alitaja asilimia 95 ya tatu ni wanaotumia dawa za kufubaza vizuri hivyo asilimia 95 wafanikiwe kuvifubaza.

Alisema wamechagua kuweka kambi katika mashindano ya mpira ya ndondo Cup kwa kuwa ni sehemu mojawapo ya kuyafikia makundi ambayo yameachwa nyuma ili kuhakikisha kwamba wanajua hali zao za maambukizi.

"Hapa tunazungumzia vijana umri kati ya miaka 15 hadi 24 lakini pia wanaume ni makundi ambayo yameachwa nyuma katika kujua hali zao za maambukizi, "alisema

**"Asilimia 95 ya kwanza ya malengo ni kwamba wale watu wote wanaoishi na maambukizi ya virusi vya Ukimwi asilimia 95 tuwe tumewafikia ifikapo 2030 na 95 ya pili ni hao ...**

Alisema, ndondo cup ni eneo ambalo linakusanya vijana linakusanya wanaume na ndiyo makundi ambayo yameachwa nyuma katika upimaji.

"Sisi tupo hapa lengo la kwanza ni kuhakikisha tunatoa uelimishaji wa kujua afya zao, hasa kujua hali ya maambunizi tunatoa huduma ya upimaji wa VVU kwa njia mbalimbali, "alisema.

Alisema huduma watakazotoa ni kutoa elimu kwa jamii ya ugonjwa huo, kuwapima afya zao na kugawa vitepe ambavyo vinawezesha wateja kujipima wenyewe na kutoa huduma ya kinga.

Alisema, elimu itahusisha matumizi sahihi ya kondomu na elimu ya namna ya kutumia dawa kinga zinazotolewa kwa wateja.

"Tutakuwapo hapa kwa muda wa mwezi mmoja na nusu na tunatarajia kuwa na michezo isiyopungua 90, tumejipanga kutoa huduma katika kila mechi tunatarajia kufikia watu wasiopungua 2,000 katika kila mechi katika viwanja vitakavyotumika," alisema.

Evangelina Chihoma, kutoka Ofisi ya Mratibu Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa kukabiliana na Ukimwi (PEPFAR) alisema wanafanya kazi zao kwa kushirikiana na Wizara ya Afya.

"Tumegundua kwamba tunatoa huduma nyingi hospitalini na kwenye jamii lakini kwa kutumia haya mashindano tunaleta zile huduma kwa vijana. Kwa hiyo, wakati vijana wanaangalia soka hapo hapo wanapata huduma mbalimbali za afya,"alisema

Hata hivyo, alisema PEPFAR imewasaidia wagonjwa takribani milioni 1.5 ambao wanatumia dawa na wanapata huduma mbalimbali ikiwamo za upimaji.

Alisema mbali na huduma za upimaji pia wanatoa dawa tiba kwa ajili ya virusi vya ukimwi, kondomu pamoja na chanjo ya saratani ya kizazi na UVIKO-19.



Balozi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert, akitoa maoni kuhusu utunzaji wa mazingira, katika kilele cha Siku ya Mazingira Duniani, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana watajwa matukio ya kujiua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Tawala Mkoa wa Dodoma, Kaspar Mmuya, ametoa wito kwa vijana kueleza changamoto wanazokabiliana kwa watu wa karibu ili kuepuka na matukio ya kujiua yanayotokana na msongo wa mawazo.

Mmuya, alisema hayo wakati wakihutubia katika maadhimisho ya siku ya kuzuia kujiua duniani yaliyoandaliwa na ofisi ya mkoa huo kwa kushirikiana na wataalamu wa afya ya akili na asasi za kiraia, yaliyofanyika katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Umonga ya jijini hapa.

Alisema tatizo la kujiua bado ni kubwa nchini huku vijana wakiongoza kukabiliwa na matukio hayo kwa kiasi kikubwa.

Mmuya alitoa wito kwa vijana kuwa wawazi kwa kuwashirikisha watu wa karibu matatizo yao kwani ndio kundi linaloonekana kukabiliwa na changamoto hiyo.

Alisema tangu mwaka 2003 dunia imekuwa ikiadhimisha siku hiyo ili kuzuia matukio ya kujiua ambayo kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), wastani wa watu 700,000 hujiua kila mwaka kote duniani.

"Hapa nchini takwimu za aina hiyo kwa miaka minne iliyopita zinabainisha kuwa vifo nane kati ya laki moja vinasababishwa na kujiua, huku nchi ambazo bado zinawatambua wanaojiua kuwa wanafanya kosa la jinai visa hivyo vikiongezeka," alisema Mmuya.

Maadhimisho ya siku hii yameongozwa na kauli mbiu isemayo, 'Badilika, anza mazungumzo yenye lengo la kuondoa ukimya na unyanyapaa'.

# Wanaotumia majibu mkemia mkuu kupotosha waonywa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

OFISI ya Mkemia Mkuu wa Serikali imekemea baadhi ya wadau wanaotumia majibu ya uchunguzi yanayotolewa na ofisi hiyo na kupotosha jamii kuwa dawa fulani inatibu ugonjwa fulani kwa lengo la kuwavutia wateja.

Mkemia Mwandamizi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ramadhani Nauja, alisema hayo jana katika Maonesho ya Saba ya Kitaifa ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yanayofanyika mjini Singida.

Alisema si kazi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuthibitisha kwamba dawa hii inatibu ugonjwa fulani bali ni kuhakikisha ubora wa dawa hiyo kwamba haina madhara kwa mtumiaji na mazingira.

"Kuthibitisha kwamba hiyo dawa inatibu kweli au laa hilo sio jukumu la Mkemia Mkuu wa Serikali. Hivyo, wadau waache kutumia majibu ya uchunguzi unaifanywa na Mkemia Mkuu kwamba dawa fulani inatibu ugonjwa fulani na imethibitishwa na Mkemia Mkuu wa Serikali," alisema.

Kuhusu maabara ya uchunguzi wa vinasaba vya binadamu, alisema kazi kubwa inayofanya ni kubaini uhalali wa wazazi, mahusiano ya kindugu, utambuzi wa watu na miili ya ambao wamepoteza maisha lakini hawajatambulika Pia, alisema wamekuwa wakipima masuala ya kitabibu mfano wanaotaka kupandikizwa figo au uroto, wanawapima kujua mahusiano ili viungo vinavyopandikizwa katika miili yao visilete madhara kwa yule anayewekewa.

"Maabara ya vinasaba vya binadamu inatusaidia kusikiliza masuala ya jinai kwa watu wanaoshiriki matukio ya uharifu, wizi, unyang'anyi na ujambazi ;hawa wote huwa tunawafanyia uchunguzi kujua nani ni mharifu,"alisema.

Nauja aliongeza kuwa sio lazima kila mtu apime vinasaba na mara nyingi wanaokwenda kupima ni wale wenye changamoto ya kutoelewana na kushindwa kukubaliana juu ya mtoto husika wakiongozwa na Sheria ya vinasaba vya binadamu namba 8 ya mwaka 2009.

Alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya uchunguzi ambao unafanyika kwa viwango vinavyotakiwa na kwa haraka, ili kwenda na kasi ya serikali katika utoaji wa haki nchini.

Alikanusha tuhuma zinazotolewa na baadhi ya watu kuwa ofisi hiyo inabadilisha matokeo ya uchunguzi, kwani wanafanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo na miongozo ya kimataifa. "Maabara ya Tanzania imepata ithibati ya ubora hivyo kinachofanyika ni kitu ambacho kinatambulika kimataifa ambapo Mkemia Mkuu wa Serikali anazo maabara sita miongoni mwa hizo ya ni kuchunguza chakula na dawa za aina zote zikiwamo za asili zinazopatikana kwenye mimea," alisema.





# Vijana waipa mbinu serikali kutokomeza tatizo ajira

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA wameiomba serikali kuzielekeza halmashauri kutenga maeneo ya kilimo kwa ajili ya kuyagawa kwa vijana wanaoingia kwenye sekta hiyo, ili kuongeza uzalishaji wa mazao na kukabiliana na tatizo la ajira.

Ombi hilo lilitolewa juzi jijini Mbeya na vijana kutoka katika mikoa tisa nchini ambao walikutana kwa ajili ya kupata mafunzo maalumu ya kuwahamasisha vijana kujiunga na sekta ya kilimo, ili wajiongezee kipato na kusaidia usalama wa chakula nchini.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Programu ya YEFFA ambayo imeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Shirika la AGRA na Master Card Foundation.

Vijana wanaoshiriki kwenye programu hiyo ni kutoka katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na mikoa ya Morogoro na Tabora, wanajishughulisha na mnyororo wa thamani wa mahindi, mpunga, alizeti na mazao ya bustani.

Mmoja wa vijana hao, Joseph Ngwale ambaye ni mkulima wa mahindi kutoka Sumbawanga mkoani Rukwa, alisema vijana wengi wanapenda kujishughulisha na kilimo lakini wanakosa ardhi kwa ajili ya shughuli hiyo.

Alisema njia pekee ya kuwavutia vijana kujihusisha na sekta hiyo ni kuwahakikishia uwepo wa ardhi pamoja na miundombinu rafiki kwenye sekta hiyo zikiwamo zana za kisasa za kilimo.

**Mratibu wa programu hiyo, Donard Mzavwa, alisema lengo la programu hiyo ni kuwafikia zaidi ya vijana 1,040,000 nchini ambao watahamasishwa kujiunga na sekta ya kilimo ..**

Naye Rehema Mbedule ambaye ni mkulima kutoka mkoani Iringa alisema mafunzo wanayopata yanawasaidia kuhamasika kuingia kwenye sekta ya kilimo lakini kama vijana hawatakuwa na uhakika wa kupata maeneo ya kilimo hayatawasaidia. Mratibu wa programu hiyo, Donard Mzavwa, alisema lengo la programu hiyo ni kuwafikia zaidi ya vijana 1,040,000 nchini ambao watahamasishwa kujiunga na sekta ya kilimo kwa ajili ya kuzalisha mazao mbalimbali ya kilimo.

Alisema kati ya vijana hao watakaofikiwa programu hiyo inalenga kuzalisha ajira 261,000 za vijana kwenye sekta ya kilimo ambao wengine watakuwa wanajihusisha na kilimo moja kwa moja na wengine watakuwa wanachakata mazao kwa ajili ya kuyaongezea thamani.

Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda alisema serikali imefanya juhudi mbalimbali za kuboresha sekta ya kilimo nchini.

Alisema serikali imegawa pikipiki kwa maofisa kilimo nchini ili kurahisisha kuwafikia wakulima pamoja na kugawa vipimia udongo kwa ajili ya kupima afya ya udongo na kuwaelimisha wakulima.

Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alisema kwa sasa sekta ya kilimo ndiyo inayoongoza kwa kutoa ajira nchini. Alisema vijana wengi wamekuwa wakiibeza sekta hiyo na kuiona kama ni utumwa jambo ambalo siyo sahihi na badala yake inasaidia kuongeza kipato kwa vijana.



Mtaalamu Mshauri wa Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Anna Kimambo (kushoto), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kwenye mkutano wa kujadili hatua zinazochukuliwa na serikali katika mradi wa kutatua migongano baina ya binadamu na wanyama kwenye ukanda wa Ruvuma. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kamati yaagiza ulinzi wa vifaa katika vituo vya afya

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Justine Nyamoga, ameagiza kulindwa kwa vifaa vyote vya ujenzi vinavyokuwapo kwenye vituo vya afya nchini.

Alitoa agizo hilo juzi wakati kamati hiyo ilipofanya ziara ya kutembelea miradi katika sekta za afya na barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe.

Nyamoga pia aliwataka wakurugenzi kusimamia miradi kwa karibu kwa kushirikiana na wananchi kwa sababu kwa kufanya hivyo itasaidia miradi kukamilika kwa wakati.

Nyamoga alisema pindi wananchi wanapoona kuna mtu anajaribu kufanya wizi watoe taarifa kwa sababu Rais Samia Suluhu Hassan analeta fedha za ujenzi na siyo kufungua duka.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI (Elimu), Zainab Katimba, alisema katika sekta ya elimu katika Jimbo la Wanging'ombe kwa kipindi cha miaka mitatu serikali imefanya uwekezaji wa Sh. bilioni nane na sekta ya afya Sh. bilioni 9.6.

Mbunge wa Wanging'ombe, Festo Dugange ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI (Afya) alisema Kituo cha Afya Wanging'ombe kinatoa huduma nzuri ya kuhudumia wananchi, hivyo serikali imetoa Sh. milioni 623 kwa ajili ya kuongeza majengo ikiwamo la huduma ya mama na mtoto.

Diwani wa Kata ya Wanging'ombe, Geofrey Nyagawa, aliiomba kamati hiyo kuongeza hadhi kituo hicho na kuwa hospitali ili kiweze kutoa huduma kubwa zaidi kwa sababu kinahudumia watu wengi ndani ya wilaya na mkoa jirani wa Mbeya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Peter Nyanja alisema halmashauri kupitia mapato ya ndani itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya umaliziaji wa miundombinu inayojengwa.

# TANESCO yawakumbuka wagonjwa hospitali sita

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Shirika la Umeme Tanzania kimetoa msaada wa mashuka zaidi ya 1,000 katika hospitali sita, lengo likiwa ni kuwapa faraja wagonjwa.

Hospitali hizo ni Mwananyamala, Temeke, Ilala, Njombe, Simiyu na Katavi, ikiwa sehemu ya kuunga mkono serikali katika kuboresha huduma za afya nchini.

Akizungumza wakati wa kutoa msaada huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, John Jingu alisema msaada huo ni nyenzo muhimu hospitalini, unasaidia kuboresha mazingira ya kazi ikiwamo huduma kwa wagonjwa.

Alisema ni jukumu la taasisi, kampuni, mashirika na jamii kuhakikisha wanalinda na kutunza maisha ya wagonjwa kwa kuhakikisha inawajali na kuwashika mikono.

"Sisi wote kama jamii tunajukumu la kuhakikisha tunawezesha kufanya kazi vizuri, serikali imefanya kazi kubwa na inaendelea kufanya kazi katika kuhakikisha inaboresha mazingira ya sekta ya afya," alisema.

Alisema Tanesco Saccos inaendelea kuleta vifaa vya kuwatia moyo wagonjwa na ni faida kubwa kwa hospitali kwa watoa huduma na watu binafsi.

Mtendaji Mkuu wa Tanesco Saccos, Andrea Hilary alisema kuna umuhimu mkubwa wa kutoa msaada huo, kwamba afya ni haki ya msingi ya binadamu na Wizara ya Afya imejitolea kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma za matibabu bora.

"Tanesco Saccos imeonyesha mfano bora wa uwajibikaji wa kijamii wa kampuni kwa kujitokeza kushughulikia baadhi ya mahitaji ya haraka katika hospitali zetu, mashuka haya tuliyotoa leo ni faraja kwa wagonjwa," alisema.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Mwananyamala, Dk. Zavery Beneath, alisema, tunafurahi kuwa kati ya wanufaika wa msaada ambapo tumepewa mashuka 200. Msaada huu utasaidia kupunguza upungufu wa mashuka kwenye hospitali."

Alisema kila kitanda kimoja cha mgonjwa kinatakiwa kuwa na mashuka nane yanayozunguka, kwamba kila yanatumika mawili.

Dk.Beneath alisema msaada huo utasaidia hospitali kuwahudumia wagonjwa kwa usahihi na viwango vinavyotakiwa vya Wizara ya Afya. Alisema uhitaji katika hospitali hiyo ni mashuka 2,400 kwa vitanda 300 ambapo kwa mzunguko kwa siku yanatakiwa mashuka nane.

# Serikali yakiri ongezeko la watoto wa mitaani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale imekiri kwamba inatambua tatizo la ongezeko kubwa la watoto wa mitaani katika eneo la Forodhani na maeneo ya mjini.

Imesema hali hiyo inaleta kero kwa wageni na wenyeji wanaotembelea maeneo hayo yenye vivutio vya utalii katika kisiwa cha Zanzibar pamoja na kuleta taswira mbaya kwa sekta ya utalii.

Soraga alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakati akijibu swali la Jimbo la Mtabwe, Dk. Mohammed Ali Suleiman, aliyetaka kujua kwa kiwango kipi serikali inalitambua tatizo hilo linalozidi kuongezeka kila siku katika maeneo hayo ya vivutio vya utalii.

Akijibu swali hilo, Soraga alisema serikali inatambua tatizo hilo na kwamba siyo kwa watoto pekee bali lipo hata kwa watu wazima.

Waziri Soraga alisema Mamalaka ya Mji Mkongwe kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya pamoja na Jeshi la Polisi inaendelea kuwaelemisha watoto wa mitaani juu ya ubaya wa tabia hiyo na kuwasihi kutafuta riziki kupitia kazi zinazokubalika kisheria.

Aidha, alisema Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mjini inaendelea na juhudi za kuwarejesha wahusika hao katika maeneo wanayoishi.

"Kutokana na juhudi hizo kwa sasa hali hiyo imepungua sana katika maeneo ya Mji Mkongwe," alisema.

Hata hivyo alisema miongoni mwa hatua wanazozichukua kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi za kuwasimamia watoto hao ili kupewa hifadhi na ulinzi unaotakwia.

Alisema hatua hizo zinaendelea vizuri na wimbi la watoto wa mtaani wanaozagaa katika Mji Mkongwe limepungua.

Alisema watoto hao pamoja na watu wazima wanaonekana katika maeneo ya Mji Mkongwe kuombaomba wengi wao ni wageni kutoka nje ya Zanzibar.

# Z'bar yakabiliwa upungufu wataalamu wa ganzi, usingizi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui amesema licha ya huduma za afya kuimarika Zanzibar, bado serikali inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa wafanyakazi wa kada za afya ikiwemo madaktari, wauguzi na wataalam wa ganzi na usingizi.

Alisema changamoto nyingine ni majengo ya hospitali ni madogo kulinganisha na huduma ambazo zinatakiwa kutolewa na Hospitali ya Wilaya.

Alitoa ufafanuzi huo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakati akijibu swali aliloulizwa na Azza Januar Joseph aliyetaka kujua ni ipi tathmini halisi ya maendeleo ya hospitali za wilaya zilizojengwa pamoja na changamoto ambazo serikali inazipitia.

Akijibu swali hilo, Mazrui alisema serikali inakabiliwa na changamoto ya usafiri kwa wafanyakazi katika baadhi ya hospitali na miundombinu ya barabara, akitolea mfano Hospitali ya Pangatupu iliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja

**Mazrui alisema pia kuimarika kwa huduma za vipimo vya maabara na radiolojia kupatikana kwa uhakika, dawa muhimu na vifaa tiba kwa zaidi ya asilimia 90 na kusogeza huduma ...**

Waziri Mazrui alisema serikali baada ya hatua iliyochukua katika kuimarisha sekta ya afya nchin ikiwemo ujenzi wa hospitali kubwa katika kila wilaya, huduma zinazotolewa katika hospitali hizo ni bora na kusababisha kuimarisha kwa huduma za afya.

Alisema huduma hizo zimesaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali Kuu ya Rufaa ya MnaziMmoja na kuimarika kwa huduma za afya ikiwemo huduma ya mama na mtoto, vyumba vya upasuaji maalum kwa ajili ya wazazi kwa kila hospitali.

Mazrui alisema pia kuimarika kwa huduma za vipimo vya maabara na radiolojia kupatikana kwa uhakika, dawa muhimu na vifaa tiba kwa zaidi ya asilimia 90 na kusogeza huduma katika maeneo ya karibu.

Alisema: "Pia kuwepo kwa huduma za dharura kwa kila hospitali, huduma za usafi, ufuaji wa nguo na chakula cha wagonjwa nazo zimeimarika".



Chumu Khamis Kombo akila kiapo kuwa Mwakilishi wa Viti Maalum Mkoa wa Kaskazini Unguja (CCM), mbele ya Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid (hayupo pichani), mjini Zanzibar jana. Kombo, anaziba nafasi iliyoachwa wazi na marehemu Panya Ali Abdallah, aliyefariki dunia, Julai mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ripoti ya Jiolojia na Utafiti wa Madini kuzinduliwa leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, leo anatarajiwa kuzindua Ripoti ya Jiolojia na Utafiti wa Madini uliofanyika Zanzibar.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduara, alisema zoezi hilo ni moja ya matunda ya makubaliano ya ushirikiano baina ya Wizara ya Nishati ya Zanzibar na Wizari ya Madini ya Tanzania bara.

Alisema kupitia utafiti huo umesababisha kuandaliwa kwa ramani ya jiolojia ya visiwa vya Unguja na Pemba ambayo hautokuwa wa awali.

Alisema Zanzibar imeshindwa kushiriki kikamilifu kwenye mnyororo mzima wa sekta ya madini kwa sababu haujawahi kunyika utafiti huo.

Aidha alisema kwa kuzingatia sababu hizo, Wizara ya Nishati na Taasisi ya Jiolojia Tanzania zimekubaliana kufanya utafiti huo katika visiwa vya Unguja na Pemba, lakini pia kwenye visiwa vidogo viliopo baharini upande wa Zanzibar, ili kuibua fursa mbalimbali za ushauri wa kitaalam.

Alisema miongoni mwa mafanikio makubwa ya utafiti huo ni kubaini maeneo yenye viashiria vya madini mbalimbali visiwani Zanzibar.

Alisema kuwa hatua hiyo itaiwezesha Wizara ya Nishati kuendelea na utafiti za kina ili kuwa na taarifa za kutosha kuhusiana na kiwango kilichopo katika madini hayo.

Alisema kuwa mbali na madini ya jiografia na jiolojia ya Zanzibar ramani ya iliyochorwa inaweza kuibua vituo vya utalii wa jiolojia na kuvitolea maelezo ya kina kwa kuwa visiwa vikubwa na vidogo ni matokeo ya mabadiliko ya kijiolojia.

Aidha alisema kuwa utafiti huo umebaini maeneo ya visiwa vya Zanzibar vyenye jiolojia kubwa na majanga ya asili kama kudidimia kwa ardhi.

"Zoezi hili ni moja ya hatua muhimu za kuunga mkono jitihada za Dk.Mwinyi katika kutekeleza ilani ya CCM kutaka rasilimali zilizopo Zanzibar kutambulika na kutumika kwa manufaa ya wananchi wote," alisema Kaduara.

Alisema lengo la kufanyika kwa utafiti huo ni kujiweka sawa na kutumia viashiria vilivyobainika ili Zanzibar isifike katika athari hizo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**BRIAN HERMAN MOLLEL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3948-0112** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ENDUIMET SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/24763/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHARLES S MBISE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0687-0060** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIKATITI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/SIN/SIN/3560/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**BAHATI ENOCK SOKOLO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA **TAE670364** ILIYOTOLEWA NA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUPITIA MAMLAKA YA UHAMIAJI HIVYO KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA: **PHQ/SON/MOM/6411/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI (ACCADEMIC TRANSCRIPT)



**NDUGU RAY GODWIN MTANGI**
Anatangaza kupotelewa na cheti (Academic Transcript) cha kuhitimu Shahada ya kwanza chenye usajili Index NO. **2112/T.93** kilichotolewa na Chuo Kikuu Sokoine (SUA) Yeyoteatakayekionaatoetaarifakituoc hochote chapolisi. Taarifapolisi: **PHQ/SIN/MAN/757/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YADON MTARIMA KOHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **LANDROVER** yenye usajili namba **T 503 ADH .** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/195396/2024**

## VIWANJA VINAUZWA

1. KIWANJA **SQM1698** CHA KUJENGA HOTEL KINAUZWA MEDELI WEST, DODOMA MJINI JIRANI MORENA HOTEL NYUMA YA SHOPPERZ BEI TSH 185, 000,000.KINA HATI MILIKI
2. KIWANJA KIKUBWA SQM 4762 KINAUZWA KISASA DODOMA JIRANI NA BARABARA YA MOROGORO BEI TSH MIL 150,000,000

**CALL 0655660730: Instagram@dodoma_deals.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA MBEYA**

**KITUO CHA IYUNGA MKOA WA MBEYA**

**SHAURI LA MADAI/NDOA Na......33/2024**

**JINA LA MDAI: SAYI MADUHU MWANJALE**

**JINA LA MDAIWA: EZEKIEL PETER MAYANGULA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(kanuni ya 18 ya Kanuni za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**KWA:**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta Madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai:**FIKA MAHAKAMANI KUSIKILIZA SHAURI LILILOPO**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 13 Mwezi 09 Mwaka 2024 saa2:30 Asubuhi/Mchana kwa mujibu wa Madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 6 mwezi 9 Mwaka 2024

..............................
**HAKIMU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA MBEYA**

**KITUO CHA IYUNGA MKOA WA MBEYA**

**SHAURI LA MADAI/NDOA Na......32/2024**

**JINA LA MDAI: SAYI MADUHU MWANJALE**

**JINA LA MDAIWA:LUKUBA SAGUDA LIL**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA:**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta Madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai:**FIKA MAHAKAMANI KUSIKILIZA SHAURI LILILOPO**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 13 Mwezi 09 Mwaka 2024 saa2:30 Asubuhi/Mchana kwa mujibu wa Madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 6 mwezi 9 Mwaka 2024

..............................
**HAKIMU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 97 YA MWAKA 2024**
**BAINA YA**
**ROBERT NGOSI SECHEMI ................................................ MDAI**
**DHIDI YA**
**JOHN NGOSI ...............................................................MDAIWA**
**LOTWA SEMBELI**

**KWA:**
**LOTWA SEMBELI**
**POPOTE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe **26.09.2024 saa 3:00** asubuhi. Kwa ajili ya kutaja.
**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 02 ya mwezi Septemba, 2024.

..............................
**MWENYEKITI,**
**Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 21508 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE HESION MDIMU NYIKA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PAULO HESION NYIKA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 30TH day of September, 2024.

Dated at KOROGWE this 09th day of September, 2024.

..............................
RESIDENT MAGISTRATE

---

## TANGAZO LA MARUDIO YA MNADA WA HADHARA

**WAUNGWANA AUCTION MART LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd,** tunatangazia umma kuwa kutakuwepo na marudio ya mnada wa hadhara wa kuuza mali ya mdaiwa iliyowekwa dhamana ya mkopo kama ilivyotangazwa gazetini kwenye jedwali hapo chini.

| Mdhamini/ Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| MARY - STELLA PETER TEMBA | TOYOTA VANGUARD T.924 EEX | 20/09/202 | Waungwana Auction Mart Limited |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/Mdhamini/ mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**WAUNGWANA: 0713077474/0766921429**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 21768 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JOEL CHARLES KINGAZI**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MISHAEL CHARLES KINGAZI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 30TH day of September, 2024.

Dated at KOROGWE this 09th day of September, 2024.

..............................
RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 21507 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE HAPPYNESS SAMWEL CHALLENGE**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PAULO DASTAN MNGUMI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 30th day of September 2024

Dated at Korogwe this 09th day of September 2024

..............................
RESIDENT MAGISTRATE

---

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 1428/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MOHAMED SAID MTAMBO WA MAGOMENI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU YALIYOLETWA NA RASHIDA MOHAMED MTAMBO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 mwezi 09 mwaka 2024 saa 2:00 asubuhi kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 11 mwezi 09 mwaka 2024.

HAKIMU

---

**IN THE DISTRICT COURT OF RUNGWE**
**AT TUKUYU**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 22010 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE EMMANUEL ALLY MWAMFISE**

**AND**

**ALLY SEMU MWAMFISE...........................PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate ( or letter of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 07the day of OCTOBER, 2024

Dated at Rungwe this 05th day of SEPTEMBER 2024

DISTIRCT RESIDENT MAGISTRATE

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie,**
**0677 020701**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 22173 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**

**SAMSON NGUSARU MMBAGA...............MAREHEMU**

**AMANI SAMSON NGUSARU..................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 11 Mwezi OKTOBA Mwaka 2024.
Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 10 Mwezi SEPTEMBA Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA

---

**THE COMPANIES ACT (CAP 212 R.E 2002)**

**NOTICE OF FINAL MEETING OF DEMBO MICRO-CREDIT LIMITED.**

**INCORPORATION NUMBER 157366645.**

**WHEREAS on 10th JUNE 2024 the members of the Company passed a final meeting of Member's Voluntary Winding -up of DEMBO MICRO-CREDIT LIMITED.**

**NOW THEREFORE THIS FINAL MEETING PROVIDES AS FOLLOWS:-**

1. THAT: A notice of Final general meeting in a members voluntary winding up of the above mention company is hereby given, that on 10th October 2024, 10:00 A.M at its registered office, the company will hold a final general meeting for the purpose of laying the accounts showing how the wound-up of the Company has been conducted, and the property of the Company has been disposed of.
Dated this 04th September 2024.


..............................
JOSEPHAT MAGESA MBEBA
LIQUIDATOR

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kamala, Trump wapeana vijembe, shutuma, hasira kwenye mdahalo



**PHILADELPHIA, Marekani**

WAGOMBEA wa urais wa Marekani, Kamala Harris wa chama cha Democratic na Donald Trump wa Republican wamepambana vikali katika mdahalo wa televisheni uliofanyika usiku wa kuamkia jana.

Mdahalo huo umefanyika katika muda wa miezi miwili kabla ya uchaguzi wa Novemba 5, mwaka huu.

Mdahalo huo uliofanyika Philadelphia ni wa kwanza kuwakutanisha wagombea hao ambao walitumia muda mwingi wakishtumiana.

Katika mdahalo huo masuala muhimu yaliyojadiliwa ni uchumi, usalama wa mipaka na uhamiaji, sheria za utoaji mimba, mzozo wa mashariki ya kati, vita vya Ukraine na mengine ya kimataifa.

Suala la kwanza wagombea hao walizungumzia ni uchumi, Harris aliweka wazi historia ya maisha yake ya kukulia ndani ya familia ya kipato cha kati kuwaahidi wapiga kura mpango wake utakaosaidia familia za aina hiyo.

Alisema atasaidia ukuaji wa biashara ndogo na za kati pamoja na kupunguza kodi kwa familia za kipato cha wastani.

Hata hivyo, Trump alimpiga vikali mpango huo akieleza utawala wa Rais Joe Biden na Harris ambaye ni makamu wake wameharibu uchumi.

Trump alisema kiwango cha mfumuko wa bei kwa sasa nchini Marekani kinatisha na kujitapa kwamba alipokuwa madarakani kati ya mwaka 2017 hadi 2021 aliimarisha uchumi wa taifa hilo.

Harris bila kukawia alijibu kwa kusema mpango wa Trump tangu mwanzo hadi sasa ni kuwanufaisha wafanyabiashara wakubwa na ikiwa atashinda itakuwa ni janga kwa watu wa kipato cha kati na masikini.

**UTOAJI MIMBA**

Suala tete la utoaji mimba pia lilijadiliwa wakati wa mdahalo. Kamala Harris amelifanya suala la haki za wanawake kutoa mimba kuwa ajenda muhimu katika kampeni yake, alimkosoa Trump kwa msimamo wake kuhusu utoaji mimba.

„Mtu hahitaji kuiweka kando imani yake kukubali kwamba serikali na Donald Trump hawapaswi kumwambia mwanamke nini anaweza kufanya na mwili wake," alisema Harris huku akimwangalia Trump.

Akijibu kauli hiyo, Trump aliwatuhumu wanachama wa Democratic kuwa na misimamo laini mno ya kilibepali akaidai baadhi yao wanaunga mkono utoaji mimba hata wakati wa kujifungua.

Hata hivyo, Hoja hiyo ilifafanuliwa na mmoja ya waongozaji mdahalo aliyesema hakuna jimbo nchini Marekani linaloruhusu kuua mtoto akishazaliwa.

**VITA UKRAINE**

Trump alijinasibu kuwa ana uwezo wa kumaliza vita vya Ukraine na kukomesha wimbi la wahamiaji.

Akizungumzia suala la mzozo wa Russia na Ukraine ambao unaendelea kwa zaidi ya miaka miwili, Trump alisema ataumaliza ndani ya siku chache tu ikiwa atachaguliwa.

„Kama ningekuwa rais, mzozo huo usingetokea, Russia isingethubutu kamwe, ninamfahamu Rais wa Russia Vladimir Putin vizuri. Asingethubutu," alisema Trump.

Harris kwa upande wake alisema washirika wa Marekani ndani ya Umoja wa Ulaya na Jumuiya ya Kujihami ya NATO wanashukuru kwamba Trump sio rais wa Marekani kwa sababu vinginevyo, Putin angekuwa ameketi mjini Kyiv na macho yake yakitizama sehemu nyingine za Ulaya, kwa kuanza na Poland.

Alimkabili Trump kwa kumwita mwanasiasa mwongo anayependa ukaribu na viongozi madikteta.

Kwenye mzozo wa mashariki ya kati, Trump alisema kundi la Hamas lisingemudu kuishambulia Israel iwapo angekuwa rais kwa sababu alipokuwa madarakani alifanikiwa kuifilisi Iran ambayo inatajwa kuwa mfadhili mkubwa wa makundi ya wanamgambo ikiwamo Hamas na Hezbollah lenye makazi yake nchini Lebanon.

Kwa upande wa Harris alisema ikiwa atashinda atashinikiza kupatikana mkataba wa kusitisha vita, na kwamba sera yake ni kuundwa mataifa mawili ya Israel na Palestina yatakayofanya mambo yake kwa amani. Wote wawili wameonesha msimamo wa kuendelea kuisaidia Israel ili kujilinda.

**VIBWEKA NA HAMAKI**

Katika mdahalo huo, wakati mmoja Trump alisikika akisema wahamiaji wanaoingia kupitia mpaka wa kusini wa Marekani wamefurika kiasi wameanza kuiba mbwa na paka kwenye maeneo wanayofikia na kuwafanya kitoweo.

Hata hivyo, kauli za wagombea hao wawili ziliibua hali ya kutupiana vijembe na kudoboana.

Harris alifanikiwa mara kadhaa kumfanya Trump ahamaki ikiwa ni pamoja na pale aliposema wafuasi wa rais huyo wa zamani huondoka mapema kwenye mikutano yake ya kampeni kwa uchovu na kutoridhika na hotuba zake.

Hoja hiyo ilionekana kumchoma rohoni Trump , ambaye alionekana kukasirika na alimjibu Harris kuwa rekodi ya mikutano yake ni ya kihistoria kuliko ya mgombea huyo wa Democratic.



**HARRIS AZIDI KUTAMBA**

Baada ya mdahalo huo, mwanamuziki maarufu nchini humo, Taylor Swift alitangaza kumuunga mkono Kamala Harris.

Katika chapisho la Instagram, nyota huyo wa pop alisema amefanya utafiti wake na ameamua kumpigia kura Harris katika uchaguzi wa Novemba..

„Nitawapigia kura Kamala Harris na Tim Walz katika Uchaguzi wa Rais wa 2024. Ninampigia kura Harris kwa sababu anapigania haki na kwa sababu ninaamini ninahitaji shujaa wa kuzipigania." Aliandika.

Aliongeza kusema „Ninaamini tunaweza kutimiza mengi zaidi katika nchi hii ikiwa tutaongozwa na utulivu na sio machafuko,"

Swift alitangaza taarifa hiyo akiambatanisha na picha yake akionekana akiwa amebeba paka kama jibu kwa mgombea mwenza wa Trump, JD Vance.

Seneta huyo wa Ohio yuko katika msukosuko kutokana na video yake ya mwaka wa 2021 kusambaa ambayo alionekana kuwaita wanachama wa chama cha Democratic kuwa kundi la wanawake wanaomiliki paka wasio na watoto ambao wana huzuni maishani mwao.

Swift aliendelea kupongeza chaguo la Harris la mgombea makamu wa rais, Gavana wa Minnesota Tim Walz, ambaye alisema „amekuwa akitetea haki za binadamu.

Mwimbaji huyo alisema kwa kiasi fulani alihamasishwa kushirikisha uamuzi wake wa kupiga kura na umma baada ya picha ya AI, kumuunga mkono Trump iliyokuwa feki ambayo ilichapishwa kwenye tovuti yake.

*DW*

# Malindi yafurahia kuanza vizuri Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA msaidizi wa klabu ya Malindi FC, Suleiman Mohamed 'Mo' amesema ni furaha kubwa kwao kuanza ligi kwa ushindi na anamatumaini wataendelea hivyo kwenye michezo yao ijayo.

Malindi SC juzi ilifanikiwa kupata ushindi kwenye mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kuifunga Zimamoto SC mabao 2-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mohamed alisema kupata ushindi katika mchezo wa kwanza kunachangia kwa kiasi kikubwa kuamsha morali na ari ya kupambana kwa wachezaji wake.

Alisema ushindi huo utawafanya wachezaji kucheza vizuri zaidi katika mchezo wao wa pili kutokana na mafanikio ya mchezo uliopita.

Alisema mchezo huo umempa mwanga wa kukiona kikosi chake vizuri ili kujua namna gani ya kukiboresha kuelekea mchezo wao wa pili.

"Tumepata alama tatu katika mchezo huu mgumu, tulikuwa tunajua kuwa Zimamoto ni miongoni mwa timu ambazo zinafanya vizuri katika Ligi kuu ya Zanzibar, tulijipanga kutumia mfumo wa kushambulia na kujilinda pamoja," alisema Mohamed.

Wakati Malindi FC wakifurahia matokeo hayo, Kocha wa Zimamoto SC, Mohamed Hilali, alisema walipoteza mchezo huo kwa bahati mbaya.

Alisema hawezi kutoa lawama kwa wachezaji wake kutokana na kupoteza mchezo huo kwa kuwa wachezaji walicheza vizuri katika dakika zote za mchezo.

"Nisema ilikuwa bahati mbaya, siwezi kumlaumu mtu kwani walionesha jitihada kubwa sana japo kulikuwa na mapungufu kidogo"alisema Mohamed.

Hata hivyo alisema anaenda kulifanyia kazi kubwa tatizo alililoliona hasa katika safu yake ya ulinzi ambapo bado hapajakaa vizuri.

# MUDATHIR: NIMETIMIZA AHADI YANGU KWA KARIA

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Timu ya Taifa 'Taifa Stars', Mudathir Yahaya, amesema ametimiza ahadi yake kwa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, kwa kufunga bao kwenye mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Afcon 2025 dhidi ya Guinea.

Taifa Stars juzi ilipata ushindi wa mabao 2-1 mbele ya Guinea huku kiungo huyo wa Yanga akifunga bao la pili na kuwahakikishia Tanzania pointi tatu muhimu.

"Kabla ya mchezo huu tuliongea na Rais Karia akataka nimpigie simu, akimaanisha nifunge ili nishangilie kwa staili yangu ya kama napiga simu, nilimwahidi kufanya hivyo na nashukuru Mungu nimempigia simu, nimetimiza ahadi yangu," alisema Mudathir.

Aidha, alisema ushindi walioupata juzi ni wa Watanzania na ni ushindi muhimu kwenye safari yao ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali hizo za Afcon zitakazofanyika nchini Morocco mwakani.

"Tunashukuru kwa matokeo haya, ni matokeo yanayozidi kututia moyo kwenye mbio zetu za kufuzu Afcon, tutaendelea kupambana kwenye michezo ijayo," alisema Mudadhir.

Matokeo hayo ya juzi yanaifanya Stars kushika nafasi ya pili kwenye kundi lao wakiwa na pointi nne, pointi mbili nyuma ya vinara Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, nafasi ya tatu inashikwa na Ethiopia huku Guinea wakiburuza mkia wakiwa hawana pointi.

Mchezo unaofuata Taifa Stars watacheza dhidi ya vinara Congo kabla ya kuanza mzunguko wa pili kusaka nafasi ya kushiriki fainali hizo za Morocco.



Vijana wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete cha jijini Dar es Salaam wakiwania mpira wakati wa mazoezi yaliyofanyika kwenye viwanja vya kituo hicho juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Manyika Jr, Miraji waibukia Mbuni FC

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa zamani wa Simba, Miraji Athumani anayecheza nafasi ya winga na golikipa, Manyika Peter, wamesajiliwa na klabu ya Mbuni FC ya Arusha kwa ajili ya Ligi ya Championship inayotarajiwa kuanza Septemba 20.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imesema kuwa wachezaji hao ni miongoni mwa nyota wao wapya waliowasajili kwa lengo la kusaka tiketi ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Tumemsajili mchezaji Miraji Sheva, aliyewahi kuichezea Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, akizitumikia pia klabu za Lipuli, Mwadui FC na Simba, lakini sasa amejiunga na klabu yetu.

Pia tumemsajili golikipa Manyika Jr, ambaye amewahi kupitia klabu za Simba, Singida Big Stars, Dodoma Jiji na Black Army, tuna imani naye, kwa sababu ni mzoefu, tunaamini atatuvusha na kutupeleka tunapotarajia," ilisema taarifa ya klabu hiyo iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano.

Sheva, alijiunga na Simba mwaka 2019 akitokea Lipuli, lakini awali alianza kuonekana kwenye kikosi cha vijana cha Wekundu wa Msimbazi kabla ya kuibukia Toto Afrika 2015. Alizichezea pia klabu za KMC, Geita Gold na JKT Tanzania.

Manyika, mtoto wa kipa wa zamani wa Sigara, Yanga, Mtibwa Sugar na Taifa Stars, Peter Manyika alianzia soka lake kwenye kikosi cha vijana cha Simba, kabla ya kupandishwa kikosi cha wakubwa mwaka 2014, lakini hakudumu sana kwenye timu hiyo.

Wachezaji hao wataanza kuonekana pale timu ya Mbuni itakapoanza mechi yake ya kwanza ya Championship, Septemba 22 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye uwanja wa Ushirika, Moshi kabla ya kucheza mechi ya raundi ya pili, Septemba 29, kwenye uwanja wake wa nyumbani, Shekh Amri Abeid, Arusha dhidi ya Geita Gold.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**VIRGIL VAN DIJK HAONDOKI**
MKATABA wa Nahodha wa Liverpool, Virgil van Dijk unamalizika msimu ujao wa majira ya joto na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 33 amesema anataka kusaini mkataba mpya wa kusalia katika klabu hiyo hadi Kombe la Dunia la 2026. ***(Mirror)***

**JORGINHO BADO ARSENAL**
ARSENAL haiko tayari kumruhusu kiungo wa kati wa Italia, Jorginho kuondoka katika klabu hiyo, licha ya kwamba Galatasaray inaripotiwa kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kabla ya dirisha la usajili la Uturuki kufungwa.***(Talksport)***

**BARCA YAMTAKA TAH, KIMMICH**
BARCELONA ina mpango wa kutaka kuwasajili mlinzi wa Bayer Leverkusen, Jonathan Tah (28) na beki wa kulia wa Bayern Munich, Joshua Kimmich (29) ambao wote wanaichezea Ujerumani, huku kukiwa na sintofahamu kuhusu mustakabali wa beki wa Uruguay, Ronaldo Araujo mwenye umri wa miaka 25, na kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye miaka 27. ***(Mundo Deportivo)***

**PARTEY AGOMBEWA ULAYA**
ATLETICO Madrid, Barcelona na Juventus ni miongoni mwa klabu zinazomtaka kiungo wa kati wa Ghana na Arsenal, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 31. ***(Caught Offside)***

**ENRIQUE MKATABA MPYA**
KLABU ya Paris St-Germain inashughulika kuongeza mkataba wa kocha Luis Enrique, ambao wa sasa unaendelea hadi Juni 2025. ***(Fabrizio Romano)***

**DAVID KUONGEZA MKATABA**
MSHAMBULIAJI wa Canada, Jonathan David, ambaye alihusishwa na Chelsea katika katika kipindi hiki cha majira ya joto, amesema alifanya mazungumzo na „timu kadhaa" lakini alichagua kusalia Lille. ***(Athletic)***

**RABIOT AGEUKA LULU EPL**
KLABU za Manchester United na Newcastle United zote zina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Juventus msimu wa majira ya joto.***(Caught Offside)***

**DAN ASHWORTH ACHUKIZWA**
MKURUGENZI wa zamani wa michezo wa Newcastle United, Dan Ashworth ambaye sasa yuko Manchester United, amekwazwa na shutuma kutoka kwa Paul Mitchell, mrithi wake katika klabu ya St James' Park, ambaye amesema muundo wa klabu hiyo wa uhamisho „haufai kwa malengo" ya klabu. ***(Telegraph)***

**KOSTIC HUYO FENERBAHCE**
KLABU ya Fenerbahce imekubali mkataba wa kumsaini winga wa Serbia, Filip Kostic mwenye umri wa miaka 31 kutoka klabu ya Italia Juventus. ***(Tuttosport)***

**DEPAY SAFI CORINTHIANS**
FOWADI wa Uholanzi, Memphis Depay, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Atletico Madrid, amekamilisha uchunguzi wa kimatibabu na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 sasa anatazamiwa kusaini mkataba wa miaka miwili na klabu ya Corinthians ya Brazil. ***(Fabrizio Romano)***

## DONDOO ZA SOKA M... YA ULAYA



# POCHETTINO KOCHA MPYA MAREKANI

Muargentina huyo ataongoza timu hiyo kwenye fainali za Kombe la Dunia 2026 baada ya...

**NEW YORK, Marekani**

MAURICIO Pochettino ndiye kocha mpya wa timu ya taifa ya wanaume ya Marekani, Shirikisho la Soka la nchi hiyo limetangaza.

Pochettino mwenye miaka 52, alitia saini mkataba wa miaka miwili ambao utamfikisha kwenye Kombe la Dunia la 2026, ambalo Marekani inaandaa pamoja na Canada na Mexico.

Kocha huyo anachukua nafasi ya Gregg Berhalter ambaye alifukuzwa kazi baada ya matokeo mabaya kwenye Copa América msimu huu wa majira ya joto.

Pochettino atatambulishwa rasmi kesho Ijumaa mjini New York.

"Mauricio ni mshindi wa mfululizo na mwenye shauku kubwa ya maendeleo ya wachezaji na uwezo uliothibitishwa wa kujenga timu zenye mshikamano na zenye ushindani," alisema Mkurugenzi wa Michezo wa Shirikisho la Soka la Marekani, Matt Crocker katika taarifa yake.

"Rekodi yake inajieleza yenyewe, na nina imani kwamba yeye ndiye chaguo sahihi la kutumia uwezo mkubwa ndani ya kikosi chetu chenye vipaji. Tunafuraha kuwa na Mauricio tunapoanza safari hii ya kusisimua ya kupata mafanikio katika ngazi ya kimataifa."

ESPN iliripoti mwezi uliopita kocha huyo wa zamani wa kimataifa wa Argentina alikubali kuchukua kazi hiyo baada ya mazungumzo marefu na Crocker.

Crocker hapo awali alifanya kazi na Pochettino katika timu ya Ligi Kuu England ya Southampton.

Muargentina huyo amewahi kufundisha katika baadhi ya klabu kubwa duniani zikiwamo Tottenham Hotspur, Paris Saint-Germain na Chelsea.

Katika kipindi hicho, amewahi kuwafundisha baadhi ya wachezaji bora katika mchezo huo, akiwamo Lionel Messi, Neymar na Harry Kane.

Mbali na Southampton, amewahi kuinoa Espanyol ya Hispania, ambako pia alitumia muda mwingi kama mchezaji.

"Uamuzi wa kujiunga na Soka la Marekani haukuwa tu kuhusu soka kwangu, ni kuhusu safari ambayo timu hii na nchi hii ziko," alisema Pochettino katika taarifa yake.

"Nguvu, ari, na njaa ya kufikia jambo la kihistoria hapa, hayo ndiyo mambo yaliyonitia moyo. Fursa ya kuongoza Timu ya Taifa ya Wanaume ya Marekani, mbele ya mashabiki ambao wana shauku sawa na wachezaji, ni kitu ambacho sikuweza kukiacha.

"Ninaona kundi la wachezaji lililojaa vipaji na uwezo, na kwa pamoja, tutajenga kitu maalum ambacho taifa zima linaweza kujivunia."

# RONALDO AMTABIRIA MBAPPÉ KUTWAA BALLON D'OR



**MADRID,** HISPANIA

CRISTIANO Ronaldo amemuunga mkono Kylian Mbappe kuwa na mafanikio katika klabu ya Real Madrid, na kutabiri Mfaransa huyo kushinda tuzo ya Ballon d'Or mwaka huu.

Mbappe alijiunga na Madrid kwa uhamisho wa bila malipo msimu huu na mara moja alitajwa kuwa mrithi wa kiti cha ufalme kilichovunja rekodi cha Ronaldo huko Madrid shinikizo ambalo Mfaransa huyo tayari amesogea kuinua mabega yake.

Baada ya mwanzo mgumu wa kampeni za 2024/25, ambazo Mbappe alitoka bila bao katika mechi zake tatu za kwanza za La Liga na pia kuhangaika katika kiwango cha kimataifa akiwa na Ufaransa, nyota huyo wa sasa wa Madrid alipata maneno ya msaada kutoka kwa Ronaldo.

"Nadhani atafanya vizuri, kusema ukweli," alisema Ronaldo akiliambia jarida la UR. Muundo wa klabu ni mzuri, mzuri na imara. Wana kocha mkuu na rais ambaye amekuwapo miaka mingi sana.

"Sidhani litakuwa suala kubwa kwake, kwa sababu ya kipaji chake, ameonesha kila kitu ambacho kinaweza kufanya hivyo. Nadhani atafanya vizuri, kusema ukweli.

"Kwa maoni yangu, anaweza kuwa mshindi wa Ballon d'Or miaka ijayo. Yeye, pengine Erling Haaland, Jude Bellingham, Lamine Yama... Nadhani kizazi hiki kipya, wana mengi wenye uwezo, lakini naamini Mbappe atafanya vizuri sana."

# Colombia yalipa kisasi kwa Argentina

**CARACAS,** VENEZUELA

JAMES Rodríguez alifunga kwa mkwaju wa penalti na kuiwezesha Colombia kushinda mabao 2-1 dhidi ya mabingwa watetezi wa Kombe la Dunia na Copa America Argentina jana alfajiri katika mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia la Amerika Kusini.

Nyota wa Argentina ambaye ni majeruhi, Lionel Messi hakucheza ikiwa ni mechi ya kwanza kati ya timu hizo tangu fainali ya Copa America.

Yerson Mosquera alitangulia kufunga dakika ya 25, lakini Argentina walisawazisha dakika ya 48 wakati Nico Gonzalez alipotumia makosa ya safu ya ulinzi ya Colombia.

Penalti ya James ya dakika ya 60 iliwapa ushindi huo kwenye Uwanja wa Metropolitano.

Mabingwa wa Kombe la Dunia Argentina walinyanyua kombe la Copa America baada ya ushindi wa bao 1-0 dakika za nyongeza dhidi ya Colombia Julai.

Colombia, ambayo haikuwa imeifunga Argentina tangu 2019, bado haijapoteza katika mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia la Amerika Kusini.

Argentina inaongoza kinyang'anyiro hicho kwa pointi 18 baada ya mechi nane, pointi mbili mbele ya Colombia.

Timu sita bora za Amerika Kusini zitapata nafasi za moja kwa moja kwenye Kombe la Dunia la 2026.

Colombia kwa mara nyingine ilimfanya Rodríguez mwenye umri wa miaka 33 kushukuru baada ya kutoa krosi nzuri kwa Mosquera kuashiria kwa kichwa na kufungua ukurasa wa mabao.

Hilo lilisawazisha rekodi ya Carlos Valderrama ya kutoa pasi 11 katika mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia la Amerika Kusini.

Makosa ya Rodríguez yaliruhusu Argentina kusawazisha, huku Nico González akimnyang'anya mpira na kumtungua kipa Camilo Vargas.

Lakini Rodríguez alirekebisha alipomshinda Emiliano Martínez, mlinda mlango mahiri kwa penalti na kufikia rekodi ya Falcao García ya mabao 13 katika kufuzu kwa Kombe la Dunia.

# De Jong kufikiria mustakabali wake Barca

[redacted]

**BARCELONA,** HISPANIA

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Frenkie de Jong anatarajiwa kutafakari mustakabali wake katika klabu hiyo baada ya ugomvi wake unaoendelea na Rais Joan Laporta kuchukua sura mpya, ripoti imedai.

De Jong amekuwa nje kutokana na jeraha la kifundo cha mguu tangu Aprili na hadi sasa amekataa shinikizo la Barcelona la kufanyiwa upasuaji ili kuharakisha kurejea kwake, licha ya kuonywa na wasimamizi wake kwamba lazima atangaze kuwa yuko tayari kwa kocha Hansi Flick iwapo atakataa kupasuliwa.


Hili ni tukio la hivi punde zaidi katika msururu mrefu wa matukio yanayomhusisha De Jong na uongozi wa Barcelona.

Kiungo huyo kwa muda mrefu amekuwa akipinga majaribio ya klabu yake ya kutaka kumuuza na hata kugombana hadharani na watoa maamuzi wakati mshahara wake ulipovujishwa kwenye vyombo vya habari.

Kwa mujibu wa Sport, De Jong sasa yuko tayari kutathmini kuhusu mustakabali wake mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 sasa yuko katika miaka miwili ya mwisho ya mkataba wake na anaelewa nafasi ya nguvu inayoambatana na hilo.

Hataruhusu Barcelona



kumpa shinikizo au kuamuru uhamisho wake mwingine, akijua wazi kuwa anaweza kuondoka bure 2026.

Uhamisho wa bei iliyopunguzwa unaweza kuwa chaguo kwa De Jong, ambaye kunaweza kuwa na orodha ndefu ya wanaomwania.

Bayern Munich iliwahi kuhusishwa na De Jong siku za nyuma, lakini uvumi mwingi ulihusu Manchester United na uwezekano wa kuungana tena na kocha wa zamani wa Ajax, Erik ten Hag, ambaye alikiri mapema mwaka huu kwamba hakuweza kuleta mtindo wa kimbinu ambao ulimfanya kuwa maarufu kwa Old Trafford bila De Jong.

HABARI MICHEZO

# FADLU ANA MATUMAINI KUWAONDOA WALIBYA

Na Adam Fungamwango

BENCHI la ufundi la klabu ya Simba lina matumaini makubwa ya kuitupa nje ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika Al Ahly Tripoli kutokana na maandalizi waliyoyafanya.

Kocha wa klabu hiyo, Fadlu Davids, amesema lengo lao katika mchezo huo utakaochezwa Septemba 15 ni kushinda ugenini ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kufuzu hatua ya makundi.

Akizungumza alfajiri ya kuamkia jana kwenye Uwanja wa Ndege, Julius Nyerere, Dar es Salaam, kocha huyo amesema pamoja na kuwa lengo lao ni ushindi, lakini mchezo huo hautakuwa mwepesi kama wengine wanavyodhani, kwani itahitajika kazi ya ziada kutokana na wapinzani wao kuwa ni timu yenye uzoefu kwenye michuano ya kimataifa.

"Al Ahly Tripoli ni timu ngumu, yenye uzoefu na michuano ya kimataifa, tumeshaisoma jinsi gani inavyocheza, na sisi tumeshajiandaa jinsi gani ya kuikabili, tumejiandaa na mapambano ya michuano hii ya kimataifa, ila sina uhakika sana na baadhi ya wachezaji wangu walivyojiandaa na kelele za mashabiki wa timu pinzani wakiwa majukwaani, napajua Libya nimeshakwenda huko mara tatu, pia nimekutana na Al Ahly Tripoli nikiwa na Orlando Pirates," alisema Fadlu.

Alisema pamoja na yote, kinachompa imani kuondoka na ushindi nchini Libya, ni kikosi chake kuwa imara na kuwa na baadhi ya wachezaji wenye uzoefu kwenye michuano ya kimataifa, pamoja na viongozi imara wenye uzoefu wa michuano hiyo.

"Simba siku zote ni timu ya ushindi, inacheza kwa ajili ya kushinda, tuna kikosi kizuri na viongozi wenye uzoefu wa michuano hii, lengo letu ni kushinda katika mchezo wa kwanza ugenini ili kuweza kufuzu kwa urahisi katika mchezo wa pili," alisema. Beki wa timu hiyo, Shomari Kapombe, amesema tayari wamefanya maandalizi na kuzielewa mbinu walizopewa na kocha wao Fadlu jinsi ya kuwakabili wapinzani wao.

"Maandalizi yetu kuelekea mchezo huu yamekuwa mazuri sana, kitu kilichobaki ni kwenda kutekeleza tu kile ambacho mwalimu alichotufundisha kwenye uwanja wa mazoezi," alisema beki huyo mkongwe.



Baadhi ya wachezaji wa Taifa Stars wakishangilia goli la ushindi alilofunga Mudathir Yahaya kwenye mchezo wa juzi dhidi ya Guinea wa kuwania tiketi ya kufuzu fainali za Afrika 2025 nchini Morocco. **PICHA: MTANDAO**

# Mwenda atoa neno Singida Black Stars

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

BAADA ya mvutano wa muda mrefu kati yake na uongozi wa klabu ya Singida Black Stars, hatimaye beki Israel Mwenda leo anatarajiwa kuwa uwanjani kuitumikia timu yake hiyo kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC huku Kocha msaidizi, Denis Kitambi akitamba kuimarika kwa safu yao ya ushambuliaji.

Mwenda ambaye aligoma kujiunga na kikosi hicho kilichokuwa kambini na kucheza mechi mbili za Ligi Kuu akishinikiza kulipwa kiasi cha Sh. milioni 60 za ada za usajili zilizokuwa zimebakia, amesema baada ya kila kitu kumalizika leo yupo tayari kuipambania timu yake mpya.

"Maandalizi yapo vizuri, wachezaji tumeshajiandaa na mchezo wetu huo dhidi ya KMC, nachosema ni kwamba mashabiki wa Singida wamiminike uwanjani kwa wingi waje kuniona kwa sababu itakuwa mechi yangu ya kwanza kuvaa jezi za Singida, lakini timu yao itakuwa nyumbani kwa mara ya kwanza baada ya michezo miwili ya ugenini," alisema Mwenda.

Beki hiyo wa kulia, ambaye ana uwezo wa kucheza kushoto, alisusa kwenda kambini licha ya kusajiliwa na klabu hiyo akitokea Simba, ambako alivunja mkataba wake kwa Shilingi milioni 140 ambazo alipewa na klabu yake mpya ya Singida Black Stars.

Hata hivyo alihitaji kiasi kilichobaki ili ajiunge na kikosi kambini kwa madai kuwa ndiyo makubaliano yalivyokuwa.

Ingawa Singida ilikubali kuwa inadaiwa lakini ilimtaka mchezaji huyo kwanza kufika kambini ili amaliziwe ‚mzigo' wake na baada ya malumbano ya wiki nzima, hatimaye sakata hilo lilimalizika kwa Mwenda kujiunga na kambi.

Singida inacheza mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu leo baada ya kushinda michezo miwili ya kwanza mabao 3-1 dhidi ya KenGold na bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar ikiwa ugenini.

Kocha Kitambi akizungumza jana na Nipashe, alisema wamefanya mazoezi ya mwisho ili kuhakikisha wanapata pointi tatu kwenye uwanja wao wa nyumbani.

"Kwa sasa timu imekaa vizuri kuelekea kwenye mchezo huo ambao naamini utakuwa na upinzani kwa kuwa mpinzani wetu ana wachezaji wazuri," alisema Kitambi.

Aidha, alisema wameimarisha safu yao ya ushambuliaji kwa mazoezi na anaamini watakuwa wakitumia vizuri nafasi watakazozipata.

## Morocco atoa siri ushindi wa Stars

INATOKA UK. 24

huku ikiwa imetoka kubanwa mbavu nyumbani na Ethiopia waliowalazimisha kutoka suluhu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na Nipashe jana, Morocco, alisema matokeo ya mchezo wao dhidi ya Ethiopia hayakuwafurahisha lakini yaliwaongezea morali ya kusaka ushindi kwenye mchezo wa juzi.

"Baada ya mchezo na Ethiopia tulirudi kwenye uwanja wa mazoezi na kuanza kuyafanyia kazi mapungufu tuliyoyaona, lakini lazima niwapongeze wachezaji wangu kwa hali yao ya kujituma na kufuata maelekezo yote, hii ndio imepelekea tumepata ushindi huu muhimu," alisema Morocco.

Alisema matokeo kwenye mchezo dhidi ya Ethiopia yaliwaumiza sana lakini wachezaji wake wameonyesha ukomavu mkubwa kwa kupambana dakika zote 90 kwenye mchezo wa juzi.

"Japo niliamini kama tutapambana muda wote tunaweza kupata ushindi, sikutegemea wachezaji kujituma namna ile na kufuata maelekezo yangu kwa asilimia kubwa, ushindi huu umechochea morali kuelekea michezo inayofuata," alisema kocha huyo.

Magoli kwenye mchezo wa juzi yalifungwa na nyota wa Azam FC, Feisal Salum ‚Feitoto' aliyefunga bao la kusawazisha baada ya awali Stars kutanguliwa kwa bao moja, goli la pili na la ushindi lilifungwa na kiungo mshambuliaji wa Yanga, Mudathir Yahaya.

Matokeo hayo yameifanya Taifa Stars kushika nafasi ya pili kwenye kundi H wakiwa na pointi nne, pointi mbili nyuma ya vinara Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo huku Ethiopia wakishika nafasi ya tatu kwa kuwa na pointi moja na Guinea wanaburuza mkia kwa kutokuwa na pointi huku kila timu ikiwa imecheza michezo miwili.

## Yanga yajipanga kumaliza kazi ugenini

INATOKA UK. 24

13 lakini wawili kati ya hao, Yao Kouassi na Farid Mussa ni majeruhi.


Yanga iliingia raundi ya kwanza kwa kuitoa Vital'O ya Burundi kwa jumla ya mabao 10-0, ikishinda mabao 4-0 mechi ya kwanza na 6-0, mechi ya marudiano, michezo yote ikipigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam. Mshindi wa jumla kati ya Yanga dhidi ya CBE, atatinga hatua ya makundi ya ligi hiyo kubwa barani Afrika.

Michezo
Alhamisi Septemba 12, 2024
Nipashe

## Pochettino kocha mpya Marekani

UKURASA 21





Mshambuliaji wa Timu Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', Clement Mzize (kulia), akiwatoka mabeki wa Guinea kwenye mchezo wa Kundi H, kufuzu fainali za AFCON juzi usiku. Stars ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Morocco atoa siri ushindi wa Stars

## ●●●Kocha huyo ashangazwa na wepesi wachezaji wake, Rais Samia atoa neno...

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Timu ya Taifa ,Taifa Stars', Hemed Morocco, amesema kujituma kwa wachezaji na kufuata maelekezo yake muda wote wa mchezo ndio sababu ya kuibuka na ushindi kwenye mchezo dhidi ya Guinea juzi usiku.

Stars ikiwa ugenini juzi ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa ,kusisimua' wa mabao 2-1 na kuendelea kuweka hai na kukoleza mbio za kushiriki fainali za AFCON mwakani nchini Morocco.

Ushindi huo pia umepongezwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ambapo kupitia ukurasa wake wa kijamii alisema,

"Hongera kwa vijana wetu wa Taifa Stars kwa ushindi mlioupata dhidi ya Guinea katika mchezo mliocheza hapo jana (juzi), alisema Rais Samia.

Aidha, Rais Samia ameitakia mafanikio mema Taifa Stars katika michezo mingine iliyopo mbele yao ya kuwania kufuzu Fainali hizo za AFCON.

Stars juzi iliingia kwenye mchezo huo

INAENDELEA UK. 23

# Yanga yajipanga kumaliza kazi ugenini

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga kimeondoka nchini alfajiri ya kuamkia jana kwenda Ethiopia tayari kwa mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CBE huku Kocha Miguel Gamondi akipanga kumaliza kazi ugenini.

Gamondi, alisema amekiandaa kikosi chake kuhakikisha wanapata matokeo mazuri kwenye mchezo huo wa ugenini ili kutokuwa na kazi kubwa kwenye mchezo wa marudiano.

"Tumejiandaa vizuri, nataka wachezaji watumie vizuri kila nafasi ili kazi tuimalize huko huko kwao ingawa nafahamu mchezo hautakuwa mwepesi," alisema Gamondi.

Alisema wanaenda kwenye mchezo huo wakiwa na hali ya kupambana na hawatakuwa na presha yoyote.

Katika hatua nyingine, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema baadhi ya wachezaji ambao wako kwenye vikosi vya timu mbalimbali za taifa, wataungana na wenzao baada ya kumaliza kuzitumika timu zao katika michezo wa kusaka tiketi ya kufuzu kucheza AFCON mwakani nchini Morocco.

Alisema katika safari yao watatumia kiasi cha saa tatu au nne kabla ya kufika nchini Ethiopia kwa kuwa hawatounganisha ndege yoyote.

"Kikosi chetu kimetoa wachezaji 14 kwenye timu mbalimbali za taifa, hao wote wataungana na timu Ethiopia wakitokea kwenye majukumu yao, tunaenda Ethiopia tukiwa na matumaini makubwa," alisema Kamwe.

Alisema Yanga imekuwa na maandalizi mazuri licha ya kutokuwa na nusu ya wachezaji wake lakini hilo halijawasumbua.

Yanga ilibakiwa na wachezaji 11 tu kambini, kati ya 27 ambao iliwasajili kwani wachezaji 14 walikuwa wamekwenda kuzitumikia timu zao za taifa na kubakiwa na wachezaji

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042